# Nipashe

Jumanne Februari 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580500

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11

## Watiwa mbaroni tuhuma uzushi vifo vya corona

UKURASA 2



## ACT-Wazalendo yateua mrithi wa Maalim Seif

UKURASA 7



# RC azuia matangazo ya misiba

UKURASA 2

# Serikali yabainisha fursa kibao Sekta ya Madini



UKURASA 3




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akizindua rasmi Kampeni ya Weka Akiba na Ushinde iitwayo Bonge la Mpango yenye thamani ya Sh. milioni 550. Benki ya NMB imezindua kampeni ya kuwazawadia wateja wake kwa kujishindia fedha taslimu, pikipiki za miguu mitatu, gari ya mizigo almaarufu Kirikuu na Toyota Fortune mpya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# Wanasiasa, wasomi wamlilia Prof. Ndulu

UKURASA 2






**MICHEZO** **SIMBA, AL AHLY DK. 90 KUAMUA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# RC apiga marufuku matangazo ya misiba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amepiga marufuku magari ya matangazo ya misiba barabarani.

Amesema matangazo hayo yanasababisha taharuki na kukwamisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi.

Chalamila alipiga marufuku hiyo, jana, wakati wa kikao cha kujadili namna ya kupunguza vifo vya watoto wachanga katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kilichofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Alisema marufuku hiyo itaanza kutekelezwa kesho, na kwamba matangazo hayo yatatakiwa kubaki nyumbani, makaburini, makanisani na misikitini, lakini sio barabarani.

Alisema kumekuwapo na tabia ya magari ya matangazo hayo kuanza kutangaza kuanzia katika eneo la chumba cha kuhifadhia maiti hospitalini mpaka nyumbani, hali ambayo alisema inasababisha usumbufu kwa watu wengine ambao hawahusiki na misiba hiyo.

“Wafiwa wanakuwa wako nyumbani, kama ni makaburini watu wanakuwa wanakujua,” alisema na kuendelea:”

“Sasa unapotangaza barabarani unataka nani asikie? Unataka machinga, dereva daladala au nani? Sasa kuanzia Februari 24, matangazo hayo ni marufuku,” alisema Chalamila.

Alisema ameshasambaza barua kwa viongozi mbalimbali kuhusu utekelezaji wa katazo hilo, huku akishauri jamii kuacha kuifanya misiba kuwa kama sherehe, na badala yake walione kama tukio la huzuni.

Chalamila alisema mara nyingi sherehe huwa zinafanyika wakati familia inapopata mtoto, harusi na mambo mengine ya furaha, lakini siku ya msiba sio ya furaha, hivyo haitakiwi kufanywa kuwa sherehe.



Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Rukia Manduta, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa afya ya uzazi na mtoto kwa Kanda ya Magharibi inayojumuisha mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni uzushi wa vifo vya corona

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu wanne wakazi wa Kibaha kwa tuhuma za kutumia mitandao ya kijamii kueneza uvumi na kutia hofu wananchi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake, alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kusambaza taarifa za uvumi za vifo vya watu wakidai wamekufa kwa ugonjwa wa corona.

Wankyo alisema watuhumiwa hao walikamatwa baada ya kusambaza taarifa hizo kupitia kundi la mtandao wa kijamii wa WhatsApp wakiilaumu serikali kwa kutokuchukua tahadhari za ugonjwa huo.

Kamanda huyo aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Frank Nyange (47), Moses Mgao (34), wote wakazi wa Kongowe, Mohamed Lutambi (45), mkazi wa Mailimoja Tangini na Bumija Senkondo (55).

Alisema watuhumiwa hao pia wanadaiwa kulitumia kundi la WhatsApp, kutaja na kupendekeza majina ya viongozi wa serikali ambao wangetamani wafe haraka kwa corona.

“Pia, wanatia hofu kwa kutumia mitandao hiyo kuwa Watanzania walio wengi watakufa kwa sababu serikali haichukui tahadhari dhidi ya wananchi wake,” alisema Wankyo.

Alisema watuhumiwa hao waliokamatwa ni pamoja na viongozi wa kundi hilo la WhatsApp ambao wanaendelea kuhojiwa na wanatakiwa kutoa ushirikiano ili sheria ichukue mkondo wake.

Kamanda Wankyo pia alitoa rai kwa wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

Aliwataka wananchi kujiepusha na matumizi mabaya ya mitandao ikiwamo kutoa taarifa za uvumi kuhusu vifo vya watu ambazo zinatia hofu wananchi.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi alisema mtu yeyote atakayebainika kufanya vitendo hivyo viovu, atachukuliwa hatua za kisheria.


**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI YA KULIPA DENI/TANGAZO LA MNADA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia **saa 4:00 Asubuhi** na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | RASHID ATHUMAN ILOKO | Nyumba ya makazi yenye hati Na.138504 Kiwanja Na. 38 Kitalu “A” Changombe Dodoma kwa jina la RASHID ATHUMAN ILOKO |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. Box 1088**
**Dar Es Salaam**
**Mobile + 255 715-363537/766-309913**

**Au**

**Mkurugezi Mtendaji**
**Bank of Africa Plc**
**P. O. Box 3054 Dar Es Salaam**


# Wanasiasa wamlilia Profesa Ndulu

**Na Elizabeth Zaya**

GAVANA wa zamani wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Profesa Benno Ndulu, amefariki dunia, huku wanasiasa na wasomi wakibainisha namna walivyoguswa na msiba huo.

Katibu Muhtasi wake, Msafiri Nampesya, alithibitisha jana kwamba Prof. Ndulu (71) alifariki dunia usiku wa kuamkia jana katika Hospitali ya Hubert Kairuki jijini Dar es Salaam alikokuwa amelazwa.

Kwa mujibu wa msaidizi wake huyo, Profesa Ndulu alikuwa amelazwa kwa zaidi ya siku 10 kabla ya kufikwa na umauti na kwamba mipango ya mazishi inaendelea nyumbani kwake Mbweni jijini Dar es Salaam.

Msomi huyo aliyebobea katika uchumi wa kitaifa kuwahi kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), aliteuliwa kuwa Gavana wa BoT mwaka 2008, akirithi nafasi ya Daudi Ballali na kudumu katika nafasi hiyo kwa miaka 10, hadi 2018.

Kabla ya nafasi hiyo, alikuwa Naibu Gavana kwa kipindi cha chini ya mwaka mmoja, akitokea alikoajiriwa na Benki ya Dunia (WB) akiwa mtendaji mwandamizi anayeshughulikia uchumi wa Afrika Mashariki.

Katika mafanikio yake, imeorodheshwa kuwezesha kushuka kwa mfumuko wa bei nchini kufikia sarafu moja asilimia nane, kutoka asilimia 20 iliyokuwapo.

Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akimzungumzia Profesa Ndulu jana, alisema: “Kwa heri Mzee wangu Prof. Benno Ndulu. Sina nguvu za kusema zaidi ya kwa heri.

“Ninamshukuru Mola kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi nawe katika miaka minane, Ninamshukuru Mola wetu kuwa tulionana wiki chache kabla ya umauti wako. Tangulia mchumi wetu uliyetukuka.”

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kati, Lazaro Nyalandu alisema: “Ni huzuni kusikia kuwa Prof. Benno Ndulu amefariki. Moyo mzuri umeondoka mapema. Mungu akupumzishe mahali pema peponi katika ufalme wake. Poleni sana familia.”

Profesa Ndulu alizaliwa Januari 23, 1950 na safari yake ya ubobezi katika uchumi ilianzia UDSM miaka 1970 na baadaye akajiendeleza zaidi na akafanya kazi na taasisi kubwa za kimataifa.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimkabidhi Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, ufunguo wa gari aina ya Toyota Land Cruiser Pickup yenye namba za usajili PT 2615 alilolitoa kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Mtama katika Halmashauri ya Mtama, mkoani Lindi, jana. Kulia ni Mkuu wa Kituo hicho, Nyabusani Wikama. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Samia: Wekezeni kwenye madini

**Na Christina Mwakangale**

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ametoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kuwekeza kwenye sekta ya madini ambayo inakua kwa kasi nchini.

Amesema kuna haja wadau hao wa maendeleo ya uchumi kuwekeza katika sekta hiyo kwa kuwa Tanzania ni kati ya nchi zenye utajiri mkubwa wa madini aina mbalimbali, ikiwamo ya kipekee ya Tanzanite.

Samia aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam, alipofungua Kongamano la Kimataifa la Madini na Uwekezaji 2021.

Alisema sekta hiyo imeendelea kuwa kinara nchini katika uingizaji mapato na mwaka jana iliongoza kwa ukuaji wa asilimia 17.7, huku ikiongoza kwenye mauzo ya bidhaa zenye thamani kubwa nje ya nchi.

Samia alisema sekta hiyo ni kati ya zinazovutia wawekezaji na kwamba Tanzania ni kati ya nchi tano Afrika zikiongoza kwenye uzalishaji madini. Pamoja na kufanya vizuri huko, kiongozi huyo alisema kuna vikwazo vya uzalishaji na soko duniani, ikiwamo kusuasua kwa biashara ya madini.

Alisema sekta hiyo sasa inawainua wachimbaji madini tofauti na awali ambako kulikuwa na utoroshaji mkubwa na kufanya waliojiajiri kwenye sekta kubakia katika umaskini.

"Kufanyika kongamano hili na kukutanisha wadau wa sekta hii, ni jukwaa la kujulisha dunia kuhusu fursa tulizonazo za madini kuanzia uchimbaji, uchenjuaji na biashara.

"Ingawa ni kipindi kigumu katika dunia ikipitia janga la corona, ni wakati mgumu katika uchumi kwa mataifa mbalimbali. Nchi 24 zinashiriki kupitia mtandao kongamano hili," alisema.

Aliwataka washiriki wa kongamano kutumia fursa ya ushiriki kuibua kero na namna ya kuboresha sekta hiyo pamoja na kutumia fursa ya kibiashara.

"Tunawakaribisha mje kuwekeza, bado sehemu kubwa ya nchi ina hazina kubwa ya madini. Kupitia serikali, tunaweza kujenga ubia, tunaweza kufanya biashara ya madini pamoja.

"Tumeingia ubia na Barrick na sasa tuna Kampuni ya Twiga. Kampuni mbili zinakaribia kuungana nasi. Ni namna ya kutumia vizuri rasilimali zetu na kunufaika nazo, Tanzania si maskini," alisema.

Samia alisema kuwa hadi mwaka 2025, Sekta ya Madini itatoa mchango wa asilimia 10 na kwamba mwaka huu Wizara ya Madini imepangiwa kukusanya Sh. bilioni 526.7 na tayari zimeshakusanywa Sh. bilioni 360.74.

"Mjadili mambo ambayo yataendana na kufungamana na viwanda. Nchi nyingi za Afrika ikiwamo nchi yetu, zimechelewa kunufaika na rasilimali madini, tuchukue hatua madhubuti," aliagiza.

"Sasa, biashara inaimarika na hakuna malalamiko kutoka pande zote mbili. Tutashirikiana na wawekezaji wote kufanikisha ukuaji wa uchumi, tutaendelea kuboreshwa soko," aliongeza.

Alibainisha umuhimu wa wachimbaji madini wakubwa na wadogo kuzingatia sheria za nchi, kutoa ajira, kurejesha hisani kwa wananchi pamoja na kutunza mazingira kwa ustawi endelevu wa jamii.

Samia alisema kuna vikwazo kadhaa mbali na mafanikio, ikiwamo uhaba au kukosekana kwa nishati ya umeme kwenye maeneo ya uchimbaji na kuahidi utapatikanaji wake baada ya mradi mkubwa wa umeme utakaozalisha takribani megawati 4,000 utakapokamilika.

Awali, Waziri wa Madini, Doto Biteko, alisema kutokana na mafanikio kwenye rasilimali madini, Tanzania imekuwa ikialikwa kushiriki mikutano ya kimataifa na kuamua kuanzisha kongamano kama hilo kufanyika nchini tangu mwaka 2019.

Alisema kongamano hilo linahudhuriwa na nchi kadhaa za nje zikiwamo zinazowakilishwa na mabalozi na mawaziri wa sekta hiyo, kujifunza na kubadilishana uzoefu.

"Sekta hii kwa asilimia 90 inaendeshwa na watu binafsi kwa kuwa wameamua kuwekeza fedha zao katika sekta hii. Serikali lazima tuwalee, kila aliyeweka pesa yake irudi," alisema Biteko.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Barrick, Mark Bristow, alisema ana imani kuwa fursa zipo kwa vijana wa kitanzania ambao watajiunga na kampuni hiyo.

Alisema migodi ni rasilimali za kitaifa na zinahitaji kuendeshwa kwa umakini, ikiwamo kutoa ajira na kuliingizia mapato taifa.

Alisema Dola za Marekani milioni 290 zilitumika katika uwekezaji wa kandarasi kwenye migodi yake ikiwamo Bulyanhulu na North Mara kwa mwaka jana.

"Utunzaji wa mazingira na usalama wa afya tunahakikisha wafanyakazi wanakuwa salama kila siku," alisema.

# Mgomo daladala, mabasi watikisa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

KUFUATIA mgomo wa daladala na wamilikiwa na maduka katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, serikali imetoa saa 24 kuwataka wausitishe na kuendelea kutoa huduma.

Imesema watakaokaidi maagizo hayo watachukuliwa hatua ikiwamo kunyang'anywa leseni zao za biashara.

Agizo hilo limetolewa jana na Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Songea ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Cosmas Nshenye, alipokuwa akizungumza na wanahabari.

Nshenye alisema kuwa ametoa tamko kwa wafanyabiashara wote wenye maduka na vyombo vya usafirishaji wa abiria kurudisha huduma zao ndani ya muda huo, na kwamba vinginevyo watachukuliwa hatua.

"Nawaagiza ofisa wa LATRA kufuta mara moja ruti ya mabasi yote yanayotoa huduma za usafirishaji wa abiria kuanzia Songea Mjini hadi Mbinga Mjini, aidha natoa rai kwa wafanyabiashara wote wenye nia njema ya kutoa huduma za usafirishaji wa abiria kutoka Songea Mjini kwenda Mbinga waone umuhimu mara moja kuanza kufanya shughuli za usafirishaji," alisema.

Nshenye pia ameiagiza LATRA na Jeshi la Polisi mkoani humo kuweka mpango mbadala wa haraka wa utatuzi wa suala la usafiri kuhakikisha huduma za usafiri zinarudi kama ilivyo pangwa.

Kadhalika, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea na LATRA kuwachukulia hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria za leseni ikiwapo kuwanyang'anya leseni zao za biashara ambao watakaidi maelekezo ya kurudi kazini kufungua biashara zao ndani ya saa 24.

Siku 7 zilizopita, wafanyabiashara walikutana kwenye mkutano wao ambao pamoja na mambo mengine, waliazimia kuiomba serikali itengue maamuzi yaliyo tolewa kuwa mabasi yote yanayotoka au kuingia nje ya mkoa na kuishia kwenye kituo kikuu cha mabasi Shule ya Tanga ambacho kiko kilomita 17 kufika Songea Mjini.

Nipashe ilishuhudia maeneo ya Soko Kuu la Songea Mjini, Soko la Manzese pamoja na maduka katika maeneo ya Matarawe, Majengo, Mahenge, Bombambili na Mfaranyaki yakiwa yamefungwa huku daladala zote zikiwa zimeegeshwa.

Abiria wengi walikuwa wakitumia usafiri wa bodaboda, bajaji na wengine walikuwa wakitembea kwa miguu.


FSSP Field Support Services Project | Tanzania

## CONSULTANCY POSITION FOR FSSP LOCAL PROJECT MONITOR

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy Services as a Local Project Monitor to the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania. The Local Project Monitor will provide technical support and advice to Global Affairs Canada in monitoring portfolio of projects and programs in the country using feminist, participatory and bottom-up approaches in monitoring project progress and performance.

Candidates will be evaluated on the following minimum qualifications and experience:

i. Master's degree in relevant discipline from a recognized University.
ii. Five (5) years of professional work experience in monitoring development projects using feminist, participatory and bottom-up approaches in developing countries, preferably Tanzania or East Africa region;
iii. Five (5) years professional work experience as a technical expert in capacity building and continuous support to Implementing Partners (especially local NGOs and CSOs) in results-based management, monitoring and reporting activities in one or more of the following sectors: education, health, inclusive economic growth, inclusive governance;
iv. Experience in in developing and operationalizing Results Based Monitoring Plan for development work;
v. Experience in carrying out research and analysis of systemic and emerging gender equality issues and trends; and
vi. Experience of working with stakeholders from Non-Government Organization the Government at all levels.

In addition to the key qualifications above, the incumbent is also expected to demonstrate the following skills and competencies:

- Data management skills (collection, cleaning, analysis, interpretation and presentation), documentation of lessons learnt and impact stories;
- Risk management skills (identification, analysis, responses planning and monitoring);
- Strong research, analytical and writing skills;
- Advanced professional proficiency in spoken and written English – level 4 and Kwahili – level 4 as explained in **http://www.international.gc.ca/ifait-iaeci/test_levels-niveaux.aspx?lang=eng;** and
- Knowledge of gender equality and equity policy priorities and processes in Tanzania.

Interested candidates may obtain detailed description of these services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their Expressions of Interest (EoIs) ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than 07 March 2021 at 23:59 hours. Late Expressions of Interest shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

# Watendaji kortini madai wizi fedha za makusanyo

Na Thobias Mwanakatwe

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Songwe, imewafikisha mahakamani watendaji wa vijiji wawili kwa tuhuma za wizi wa zaidi ya Sh. milioni 10, ambazo ni za makusanyo.

Wakisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Songwe, Vitalis Changwe, mawakili wa TAKUKURU, Emanuel Ndembeka na Simona Mapunda, walidai kuwa kwa nyakati tofauti washtakiwa wakiwa watumishi wa umma, walitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 270 cha Kanuni ya Adhabu, sura ya 16 ya mwaka 2019.

Katika kesi namba 32 ya mwaka 2021 inayomhusu Jenson Shitindi (48) ambaye ni mtendaji wa kijiji cha Mlangali, anadaiwa kuwa kwa tarehe tofauti kati ya mwaka 2015 hadi 2020 kwa nia ovu pasipokuwa na uhalali wowote, aliiba kiasi cha Sh. 2,451,096 ambazo ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Ndembeka, alidai fedha hizo zilitokana na makusanyo yaliyofanywa kwa njia ya mfumo wa kielektroniki maarufu kwa jina la POS.

Katika kesi ya pili namba 33 ya mwaka 2021 iliyosomwa na mwendesha mashtaka wa TAKUKURU, Simona Mapunda ikimhusu mtendaji wa kijiji cha Hatelele, Shadrack Mgallah (47), ilidaiwa kuwa mtendaji huyo kwa nyakati tofauti kati ya mwaka 2017 hadi 2020 aliiba fedha za makusanyo kiasi cha Sh. 7,981,986, mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Baada ya kusomewa makosa yao watuhumiwa walikana kutenda makosa hayo na walishindwa kutimiza masharti ya dhamana, hivyo kulazimika kurudishwa mahabusu.

Hata hivyo, licha ya upelelezi kukamilika, kesi hiyo imeahirishwa hadi Machi 3, mwaka huu kwa ajili ya usikilizwaji.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, akizungumza na Watendaji Wakuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), kuhusu masuala mbalimbali ya utendaji kazi. jijini Dar es Salaam, jana. Katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, Dk. Anorld Kihaule. PICHA: WMN


UBALOZI WA DENMARK, NETHERLAND

FINLAND NA UINGEREZA
DAR ES SALAAM

MNADA WA HADHARA:

UNIVERSAL AUCTION CENTRE Kwa idhini waliyopewa na Ubalozi wa Denmark, Netherlands, Finland na Uingereza watauza kwa mnada wa hadhara Magari,Majenereta,Pikipiki na Funicha za nyumbani tarehe 27 February, 2021 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

Fenicha zitaanza kuuzwa saa 4:00 asubuhi: Sofa beds, Chest drawer, Dressers, Makabati, Meza za chakula, Viti, Meza za ofisi, Viti, Book case, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, Majiko ya umeme na Gas, TV , A/c split units, Photocopy m/c, Water Pump, Tyres za magari , Laptop, Computer set na vingine vingi. Magari na Generator yataanza kuuzwa kuanzia saa 6.00 mchana.

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | L/ Rover Freelander S.Wagon | 4 Cylinder Petrol Engine | 2012 | Bado |
| 1 | Ford FIGO Saloon | YFAA Petrol Engine | 2012 | Bado |
| 1 | Ford Ecosport Station Wagon | 9BFUT Petrol Engine | 2015 | Bado |
| 1 | Nissan Murano Station Wagon | JNIT QR25 Petrol Engine | 2006 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Land Cruiser Prado | VZJ Petrol Engine | 2004 | Umelipwa |
| 1 | Mazda Atenza Saloon | GG3S Petrol Engine | 2002 | Umelipwa |
| 3 | Honda &Yamaha Motorcycles | XL 125 & YBR125G Petrol | 2010 | Bado |
| 3 | Generator Silence 30 Kva | Perkins Engine Diesel | 2012 | Bado |

MASHARTI YA MNADA.

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari/Generator atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 4 March, 2021 saa 10:00 jioni, ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Generator litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.

2 Malipo kwa njia ya VISA na Master cards za CRDB na NBC bank yanakubalika.

3 Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.

4 Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.

5 Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi

6 Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

7 Kila mtu atatakiwa kuchukua tahadhari ya Corona kwa kuvaa Barakoa.

Kwa maelezo zaidi waone:
UNIVERSAL AUCTION CENTRE
PLOT NO: 5 "E" LION STREET SINZA
CELL NO: 0754 284 926, 0757 284 926 Instagram: universalauctioncentre
E-mail: universalauction@hotmail.com DAR ES SALAAM


# Viwanda, kilimo vilivyoipaisha Tanzania

Na Mwandishi Wetu, MTWARA

SEKTA za ujenzi, kilimo na viwanda zimechangia Tanzania kuingia katika uchumi wa kati kutokana na kuongezeka kwa mchango wake kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi 2019.

Aidha, sekta nyingine ni usafirishaji na uhifadhi mizigo na biashara, ambazo ziliwezesha kuimarika kwa uchumi kwa kuongeza kipato cha wananchi.

Akiwasilisha mada ya mapito ya hali ya uchumi nchini katika semina ya waandishi wa habari za uchumi, biashara na fedha, Meneja Msaidizi wa Uchumi na Takwimu wa Banki Kuu ya Tanzania (BoT), Aristeded Mrema, alisema sekta hizo zinagusa maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Alizitaja sekta hizo na asilimia zake kwenye mabano ni ujenzi (25), kilimo (20), viwanda (9.6), usafirishaji na uhifadhi mizigo (8.3) na bishara (7.3).

Kuhusu mwenendo wa uchumi, alisema unaonyesha kuwa wastani wa kipato kwa kila Mtanzania uliongezeka hadi kufikia wastani wa Dola za Marekani 1,080 mwaka 2019, ikilinganishwa na Dola za Marekani 980, mwaka 2015.

Aidha, kuna kuongezeka kwa kipato ambako kumepunguza idadi ya watu walio maskini nchini, kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/2012 hadi kufikia asilimia 26.4 mwaka 2017/18.

"Uchumi umeendelea kuwa imara katika kipindi cha robo tatu za mwanzo za mwaka 2020 licha ya athari za janga la corona lililoikumba dunia," alisema.

Kwa mujibu wa Mrema, pato la taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 4.7 katika miezi sita ya kwanza ya mwaka 2020, ikilinganishwa na asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2019 na asilimia 6.9 mwaka 2018.

"Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchukuzi na uchimbaji madini. Pia uamuzi wa serikali kutofunga shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa corona," alisema na kuongeza:

"Ukuaji huo ulitokana na uwekezaji ambao serikali imeendelea kufanya katika miundombinu, ukichangia na utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi na sera madhubuti ya bajeti ya serikali."

Kwa mujibu wa meneja huyo, matarajio ya ukuaji wa uchumi unakadiriwa kuwa ni asilimia 5.5 mwaka 2020 na asilimia 6 au zaidi mwaka 2021.

Nyingine ni sera ya fedha yenye kulenga kuongeza ukwasi na kuongezeka kwa wawekezaji katika sekta binafsi.

Kuhusu mfumuko wa bei, alisema umeendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 5 kwa mwaka, na kwamba kwa kipindi cha miaka mitano ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.2. Kuhusu mikopo ya benki kwa sekta binafsi, alisema iliongezeka na kukua kwa wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2019/20, ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2018/19.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa awakabidhi magari polisi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekabidhi magari mawili kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi mkoa wa Lindi, yatakayowezesha askari kutoa huduma katika maeneo ya mkoa huo.

Alikabidhi magari hayo jana, baada ya kuzungumza na wananchi katika kituo cha Polisi Mtama ambako makabidhiano hayo yalifanyika.

Magari yaliyokabidhiwa ni Toyota Land Cruiser Pickup yenye namba za usajili PT 2615 na Toyota Land Cruiser V6 lenye namba za usajili PT 4378.

Kati ya magari hayo gari moja TP 4378 ni kwa ajili ya ofisi ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Lindi na gari lingine PT 2615 ni kwa ajili ya Kituo cha Polisi cha Mtama.

Waziri Mkuu alisema serikali itaendelea kutoa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi kadiri inavyowezekana ili kuwawezesha askari kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Akizungumza baada ya kupokea magari hayo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Lindi, Mtatiro Kitinkwi, alisema magari hayo yatawezesha shughuli za doria kufanyika kwa uhakika.

"Magari haya unayotukabidhi leo (jana) yatawezesha shughuli za usafiri wa polisi, doria na usafirishaji wa mahabusu kufanyika kwa uhakika kulingana na jiografia ya Halmashauri ya Mtama."

Kamanda Kitinkwi aliiomba serikali kukimalizia Kituo cha Polisi cha Mtama kwa kuweka samani na kujenga kambi ya makazi ya askari katika kituo hicho.

Naye Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye, kwa niaba ya wananchi aliishukuru serikali kwa kutoa magari hayo ambayo yatawezesha shughuli za ulinzi na usalama katika jimbo hilo na Mkoa kufanyika kwa ufanisi zaidi.

## Mkoa waja na mkakati wa kuzalisha mkonge

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI mkoani Morogoro imeanza mkakati wa kufufua zao la mkonge kwa uhamasishaji wakulima, kuanzia utambuzi wa mashamba yasiyoendelezwa.

Katibu Tawala wa Mkoa huo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, alisema hayo mjini Morogoro mbele ya Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, kuhusiana na sekta ya uchumi na uzalishaji mali kupitia kilimo.

Kalobelo alisema mkoa huo una jumla ya mashamba makubwa sita yenye ukubwa wa hekta 19,834 kati ya eneo hilo linalolimwa ni hekta 7,573, na wakulima wadogo 14 wenye mashamba yenye ukubwa wa hekta 245.

Alisema zao la mkonge lilikuwa linalimwa katika halmashauri za Kilosa na Morogoro, lakini kutokana na uhamasishaji uliofanyika na viongozi, kwa sasa halmashauri za Gairo na Mvomero nazo zimeanza kulilima.

Alisema katika kuendeleza zao hilo, Halmashauri za Gairo na Morogoro zimeanzisha vitalu vya miche 32,000.

"Tumeanza shughuli za uhamasishaji na kufanya mafunzo ya kilimo cha zao la mkonge kwa wataalamu wa kilimo 83 na wakulima 104, na uzalishaji wa vitalu vya miche ya mkonge umefanyika," alisema Kalobelo.

Alisema mkoa umeamua kuwapanga maofisa ugani katika maeneo yanayolimwa mkonge ili wakulima wapate ushauri wa kilimo na hatimaye wazalishe kwa tija.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusiwe 'veterani' wa corona tuwasikilizeni wataalamu

**WAKATI** wakuu wa serikali wanatafuta njia ya kusaidia watu wasipate taharuki kisaikolojia na kiuchumi kutokana na changamoto ya corona, ni vyema viongozi wakiwamo wakuu wa mikoa, wilaya, mitaa na wenye majukumu ya afya kuwahamasisha wananchi kujikinga na kuondoa dhana na maelezo mengi potofu yasiyo na tija.

Tunasema haya kwa sababu wapo vijana na hata baadhi ya watu kwa mfano wanaoendelea kusema kuwa corona ni ugonjwa wa wazee na wenye maradhi sugu na kwamba hauwapati vijana na hili linadhihirika miongoni mwa vijana hasa wanaoendesha bodaboda na bajaji.

Licha ya kukutana na abiria wengi wakiwamo wagonjwa na wanaowahudumia wanaoumwa corona, madereva hawa hawatumii barakoa na kinachoonekana ni kukosekana uhamasishaji. Haya ni mambo ambayo hayana maana. Aidha, wapo wanaowaambia watu kuwa barakoa hazisaidii. Hivi ni vitu ambavyo vinatakiwa kukwepwa na umma kuhamasishwa kwa nguvu zaidi.

Tunategemea kuwaona viongozi wakuu wakitoka ofisini na kusimamia usafi kuanzia kwenye vituo vya mabasi, mikusanyiko masokoni, minadani, kwenye kumbi na popote panapohitajika kuwa na usimamizi na ufuatiliaji ili kulinda maisha.

Ukweli ni kwamba maradhi yapo kama Rais John Magufuli, alivyosema hivyo ni lazima kuchukua tahadhari na kuzingatia maelekezo ya wataalamu na kuendelea kujiongeza kwa kujitakasa kuepuka ugonjwa huo.

Kwa mfano, pamoja na kunawa mikono kila wakati, kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na kukaa umbali wa mita moja kutoka mtu hadi mtu pengine ni vyema kuacha kukaa kwenda kwenye mikusanyiko isiyo na ulazima.

Aidha, ni wakati wa wenye daladala na wanaosafirisha abiria mijini kuacha kujaza abiria jambo ambalo linaweza kusababisha kasi ya kusambaa kwa magonjwa hasa mijini. Lakini ni vyema kukumbushana kuvaa barakoa hasa kwenye magari hayo kwa sababu kukinga ni bora kuliko kuponya.

Kuwahamasisha wananchi kubadili tabia na kufahamu kuwa kuingia kwenye maisha mapya. Tunategemea sasa tuone matangazo ya kuhamasisha watu kuvaa barakoa, kubadilisha nguo walizovaa wakiwa sokoni, kanisani na kazini wanapofika nyumbani na ikiwezekana kuoga mara moja ili kujiweka kwenye hali ya usalama zaidi.

Tunarajia pia kusikia watu wakikumbushwa kuacha kujimezea dawa kama wanavyopenda maana kuna wanaokula dawa (antibiotics) kila mara kujikinga, wapo wengine wanaomeza vidonge vya kuongeza kinga ya mwili. Hili ni jambo la kuangaliwa pia. Si afya kutumia dawa kwa muda mrefu bila ulazima na maelekezo ya madaktari.

Tunaikumbusha serikali hili nalo kulikemea na kuonya kwa vile kuna uwezekano wa kujenga usugu miongoni mwa Watanzania ambao pengine hawatapata corona, lakini wakawa wamekunywa dawa nyingi bila sababu.

Tunasema hayo kwa sababu kuna maelezo mengi kuhusu tiba ya corona yanayotolewa mitaani na mengine yanatekelezwa na baadhi ya wataalamu kwenye maduka ya dawa wanaowahimiza watu kutumia dawa za aina fulani kwa maelezo kuwa zinaongeza tiba.

Tunapenda kuwakumbusha watu kutumia vyakula na tiba za asilia ambazo zimeelezwa mara kwa mara na wataalamu wa dawa nchini zikihusisha kula ndimu, tangawizi, limau, nanasi, machungwa, matunda yenye rangi ya njano, karoti, mboga za majani na pia kujifukiza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Wenye wastani wa D wakisaidiwa wanaweza

**NI** vurugu zilizotulizwa na askari polisi kwa kutumia gari la maji ya kuwasha kutawanya mashabiki.

Mashabiki wa Yanga na Mbeya City wote walikuwa wakimlaumu mwamuzi Ludovic Charles kuwa hakuwatendea haki huku wale wa Mbeya City wakimlaumu mwamuzi huyo kwa madai kuwa aliwapa Yanga bao ambalo kwao waliamini mpira haukuvuka mstari.

Hilo lilikuwa ni bao la Deus Maseke kwenye dakika ya 85 ambalo pamoja na kuokolewa na Babilas Chitembe, lakini mpira tayari ulikuwa umevuka mstari wa goli.

Nao mashabiki wa Yanga walikuwa wakiilalamikia penalti walioipata Mbeya City kuwa haikuwa halali. Lakini ukiangalia marudio ya picha za video inaonekana bao la Yanga lilikuwa ni sahihi. Mpira ulikuwa umevuka mstari. Na hata penalti iliyopatikana kwa Mbeya City ilikuwa ni halali kwa sababu inaonekana kabisa mpira umemgonga mkononi beki, Yassin Mustapha.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze na Kocha Mkuu wa Mbeya City, nao pia wakaingia kwenye mtego wa mashabiki wao. Nao, pamoja na mambo mengine, wakamlaumu mwamuzi huyo kwa kila mmoja kudai kuwa timu yake haikutendewa haki.

Hata hivyo, ukiangalia uchezeshaji mzima wa mwamuzi huyo huoni kosa lake. Kila kitu kilicholalamikiwa hakikuwa sahihi. Labda ni makosa machache tu ya kawaida ambayo yapo kwa kila mwamuzi. Lakini goli la Yanga na penalti ya Mbeya City, vyote vilistahili. Tatizo ni kwamba makocha na mashabiki wao walitaka moja wapo kati ya hilo lisiwapo kwa wapinzani wao. Yanga walitaka bao lao liwe sahihi, lakini penalti isiwe sahihi. Mbeya City nao walitaka penalti yao ikubaliwe, lakini si bao la Yanga.

Ukichanganya na kuwa mabao hayo yalifungwa dakika za mwisho ndiyo kabisa yalizidi kuwachanganya mashabiki hao. Bao la dakika tano kabla mechi kumalizika, na la dakika tatu za nyongeza lililofungwa kwa penalti na Pastory Athanas, liliwafanya mashabiki kupagawa na kushindwa kuamini kinachotokea uwanjani.

Nadhani mashabiki wa Yanga baada ya bao lile, walidhani kazi imekwisha, bila kujua kuwa mpira wa miguu hauishi mpaka filimbi inapopulizwa.

Nafasi ambayo Yanga ipo, na ile ambayo Mbeya City ipo, ndiyo ilisababisha jazba kwa mashabiki wa timu zote mbili.

Yanga ipo kileleni ikiwa na pointi 45. Kabla ya mechi hiyo ilikuwa na alama 44 na ilizihitaji pointi tatu kwa udi na uvumba ili izidi kuikimbia Simba yenye pointi 38, hasa baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 hivi karibuni dhidi ya Azam FC.

Mbeya City iko kwenye hatari ya kushuka daraja ikiwa na pointi 15, nafasi ya 17. Na kabla ya mechi hiyo ilikuwa na pointi 14, hivyo ilihitaji pointi tatu ili kujivuta juu kidogo ya msimamo. Ndiyo maana utaona kila timu ilikamia na kuzitaka pointi tatu kwa udi na uvumba.

Ninachokiona hapa ni kwamba timu zote hizi zina upungufu makubwa ambayo wanayaficha kwa kivuli cha mwamuzi.

Mbeya City iko nafasi moja tu kutoka mkiani. Inashangaza kwani kwa mpira iliyocheza jana, ni ajabu kuona inadondosha pointi nyingi ikicheza na timu nyingine.

Kwenye mechi 19, Mbeya City imeshinda mbili tu, sare tisa na kupoteza nane. Hapo ndipo viongozi, makocha, wachezaji na mashabiki wa Mbeya City ilibidi watatue tatizo na si kumlaumu mwamuzi ambaye alionekana kuumudu mchezo huo.

Kwa upande wa Yanga, kocha Kaze anatakiwa kuinoa safu yake ya ushambuliaji ambayo inaonekana ni butu na si kuanza kumlaumu mwamuzi.

Kama washambuliaji wa Yanga wangekuwa makini, wangefunga mabao zaidi ya matatu, na lile la Mbeya City ingekuwa tu la kufutia machozi, lakini inaonekana kuwa imekuwa sasa ni tabia ya Yanga kufunga bao moja kwenye mechi nyingi, ikidhani inatosha kumaliza mechi.

Mimi nadhani timu hizi na makocha wake, wanaficha upungufu yao kwa kumlaumu mwamuzi ambaye hakuwa na baya kwenye mechi hiyo na kama yapo basi ni madogo ya kibinadamu lakini si kwa mabao hayo ya pande zote mbili.

# Maalim Seif apata mrithi

**Na Maulid Mmbaga**



CHAMA cha ACT-Wazalendo kumemteua Dorothy Semu kukaimu nafasi ya uenyekiti wa Taifa, nafasi iliyokuwa inashikiliwa na Maalim Seif Sharif Hamad, aliyefariki dunia wiki iliyopita.

Maalim Seif, ambaye alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alifariki dunia Jumatano alipokuwa amelazwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) jijini Dar es Salaam.

Kiongozi huyo alizikwa Alhamisi kijijini kwake Mtambwe, kisiwani Pemba, kwa heshima zote za kiserikali.

Semu kabla ya kuteuliwa kushika wadhifa huo, alikuwa ni Makamu Mwenyekiti Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Habari wa chama hicho, Salim Bimani, hatua hiyo imefikiwa kwa mujibu wa ibara ya 84(3) na (4) ya Katiba ya ACT ya Mwaka 2015 toleo la 2020.

"Ibara 84(3) inasomeka iwapo mwenyekiti wa chama hayupo kwa sababu yoyote ile, basi makamu mwenyekiti ambaye anatoka upande mwingine wa muungano tofauti na anaotoka mwenyekiti, na kama aliyetajwa kwanza naye hayupo, basi aliyebakia atakaimu nafasi ya uenyekiti," alisema.

Aidha, kwa kuzingatia Ibara ya 84(4) ya Katiba ya ACT, Semu ataendelea kukaimu nafasi hiyo kwa kipindi kisichozidi miezi 12 hadi pale mwenyekiti mpya atakapochaguliwa na mkutano mkuu maalumu wa Taifa.

## Taasisi yaagiza vijiji, mitaa kupinga mikopo inayoumiza

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Dodoma, imewataka viongozi wa kata na vijiji kutoa elimu kwa wananchi kuhusu mikopo umiza inayotolewa na watu mbalimbali ili waiepuke.

Pamoja na kuikataa wananchi watakwepa rushwa na dhuluma nyingine zinazoambatana na upatikanaji wa fedha katika maeneo mbalimbali wanayoishi.

Kauli hiyo imekuja baada ya uchunguzi wa TAKUKURU kubaini baadhi ya wananchi wasio na uelewa kuhusu vitendo vya rushwa wamekuwa wakidhulumiwa haki zao kutokana na fedha za mikopo umiza.

Mikopo hiyo wanaichukua kutoka sehemu mbalimbali zikiwamo taasisi na watu binafsi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma Sosthenes Kibwengo, alisema viongozi wanapaswa kuwaelimisha wakazi wa maeneo yao kusaidia kupunguza dhuluma zinazofanywa na watoa mikopo umiza.

"Tunawatahadharisha watu wanaokopesha fedha jijini hapa kuacha tabia ya kuwatoza wananchi riba kubwa, badala yake wafuate sheria, kanuni na taratibu za nchi zinazotumika kukopeshana pesa," alisema.

Kibwengo alisema viongozi katika ngazi mbalimbali jijini hapa hususani waliopo pembezoni wanapaswa kutafuta mamlaka husika kutoa elimu ya mikopo kwa wananchi ili kuwasaidia kutodhulumiwa haki zao za msingi mara wanapochukua mikopo yao na kushindwa kurejesha kwa wakati kutokana na riba kubwa wanazokutana nazo.

Akizungumzia mikakati ya TAKUKURU ya kutembelea maeneo mbalimbali waliojiwekea kusikiliza kero za uunganishaji umeme, Kibwengo alisema wamepanga kila Jumanne ya kwanza ya mwezi kutembelea sehemu hizo kwa ajili ya kusikiliza kero za uunganishwaji umeme.

Alisema wameshapita katika kata ya Ng'ong'ona na walisikiliza wananchi wa maeneo hayo na kubaini wengi wa wakazi wa maeneo hayo hupotoshwa kuhusu taratibu za kuchukuaji fomu ambazo hutolewa bure na TANESCO.

Alisema wataendelea na kampeni hiyo katika maeneo mengine kusikiliza kero hizo ili kuhakikisha wananchi kupata haki zao za msingi kwenye mpango wa kuunganisha umeme.

Alisema wamepanga kufanya hivyo ndani ya miezi mitatu mfululizo kwa imani kuwa wananchi watapata uelewa kuhusu vitendo vya rushwa kwenye kuunganishiwa umeme katika maeneo mbalimbali jijini.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUWEKEZA KWENYE ENEO LA BADECO (Marudio),**

**UBINAFSISHAJI WA HUDUMA ZA USAFI NA ULINZI**

**22/02/2021**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inawatangazia wafanya biashara, Kampuni au watu binafsi wenye uwezo wa kuwekeza kwenye eneo la iliyokuwa Bagamoyo Development Corporation ( BADECO) ambalo sasa ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Eneo hilo lina ukubwa wa hekta 1.889, ndani yake kuna magofu ya iliyokuwa BADECO Hotel na lipo ufukweni Bagamoyo kando ya Bahari ya Hindi. Ni eneo zuri, lenye kuvutia, kufaa na kuburudisha kwa watu wanaopenda kuona mandhari ya bahari, kuogelea, kupata upepo mwanana wa baharini, kufanya sherehe, kufanya utalii wa baharini, kuona mambo ya kale yanayozunguzuka eneo hilo pamoja na kupata burudani nyingine nyingi zinazopatikana ufukweni hapo.
2. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inazitangazia Kampuni au vikundi vilivyosajiriwa kwa ajili ya kutoa huduma za usafi na ulinzi katika ofisi na majengo yake kwa kipindi cha Julai 1, 2021 hadi Juni 30, 2022.
3. Namba za zabuni husika na maelezo yake mafupi ni kama ilivyooneshwa katika jedwali lifuatalo hapa chini:-

| NAMBAYA ZABUNI | MAELEZO YA ZABUNI |
|---|---|
| LGA/014/2021/2022/HQ/BADECO/01 | Zabuni ya uwekezaji katika eneo la ufukweni la iliyokuwa BADECO Hotel |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/01- LOT 1 | Zabuni ya huduma za Usafi katika ofisi za idara na vitengo na mazingira ya makao makuu ya Halmashauri |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/01- LOT 2 | Zabuni ya huduma za Usafi katika ofisi, vitengo na mawodi ya Hospitali ya Wilaya |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 1 | Zabuni ya huduma ya ulinzi katika ofisi, majengo mbalimbali ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na majengo ya JICA na Nanenane Morogoro. |
| LGA/014/2021/2022/HQ/N/02- LOT 2 | Zabuni ya huduma ya ulinzi katika Hospitali ya Wilaya |

**4. MASHARTI KWA MWOMBAJI/WAOMBAJI**

(i). Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

(ii). Mwombaji alipe ada ya maombi ya zabuni ya Tshs. 100,000/= ambazo hazitarudishwa.

(iii). Mwombaji awe na Leseni hai ya biashara pamoja na hati ya ulipaji kodi: TIN/VAT

(iv). Mwombaji ambaye ni kampuni au kikundi awe na Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni au kikundi.

(v).Mwombaji awasilishe Memorandum and Articles of association/Extract from the Register kama ni kampuni au joint venture.

(vi).Mwombaji aambatanishe Bank statements za miezi mitatu ya Novemba na Desemba 2020 na Januari 2021

(vii).Mwombaji wa kuwekeza katika eneo la BADECO atembelee eneo hilo, aandae andiko la jinsi anavyotarajia kuwekeza katika eneo hilo na ataje kiwango atakachoilipa Halmashauri kwa miezi mitatu, miezi sita au mwaka wakati akirejesha gharama zake za uwekezaji. Namna ya kutembelea eneo hilo la BADECO imeelezwa katika kipengele Na 5 cha tangazo hili.

(viii) Mwombaji wa kutoa huduma za ulinzi awe na kibali cha kufanya hivyo kutoka kwenye jeshi la Polisi ( Wizara ya Mambo ya ndani).

(ix).Maombi yaambatane na Dhamana ya Zabuni (Bid Security) katika muundo wa bid securing declaration.

(x).Dhamana ya utendaji "Performance Bond" ya 10 % ya thamani ya mkataba italipwa na mzabuni kabla ya kusaini mkataba kwa mzabuni atakayeshinda

(xi). Mwombaji ambaye ni kampuni au kikundi aambatanishe Special Power of Attorney ya mtia Saini wake.

(xii). Mwombaji ataje eneo atokako au ofisi ya kampuni ilipo (physical address), anwani yake pamoja na simu ya mkononi na barua pepe (e-mail) kama anayo kwa ajili ya mawasiliano.

5. Vitabu vya zabuni na maelezo zaidi vinapatikana katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(w) Bagamoyo kitengo cha Ununuzi na Ugavi kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri siku za kazi (Jumatatu hadi Ijumaa)

6. Nyaraka za maombi ya zabuni hii ziwe katika nakala mbili: nakala moja iwe halisi na nyingine iwe nakala kivuli. Nakala zote mbili zifungwe kwa LAKIRI, na kuwekwa kwenye bahasha kubwa itakayoandikwa "NAMBA NA JINA LA ZABUNI ILIYOOMBWA"na kutumbukizwa katika sanduku la zabuni lililoko Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo baada ya kuorodheshwa kwenye rejesta ya kupokelea maombi ya zabuni iliyopo kwenye ofisi ya Kitengo cha Ununuzi na Ugavi. Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

**KATIBU**
**BODI YA ZABUNI HALMASHAURI YA WILAYA**
**S.L.P 59, BAGAMOYO**

7. Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 09/03/2021 saa tano na nusu asubuhi (5.30). Maombi zabuni yatafunguliwa muda mfupi baadaye katika ukumbi wa mikutano Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya na waombaji wanakaribishwa katika ufunguzi kwa gharama zao.

8. Maombi ya zabuni ambayo yatachelewa kuwasilishwa ndani ya muda uliotajwa hapo juu hayatakubaliwa kwa namna yoyote ile.

*FATUMA O. LATU*

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO**

# Waziri aagiza kodi ya ardhi, majengo

**Na Munir Shemweta,** SONGWE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ametaka zoezi la utambuzi wa wamiliki wa nyumba liende sambamba na kutambua viwanja visivyolipiwa kodi ya pango la ardhi.

=Alitoa kauli hiyo jana, wakati akizungumza na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Songwe pamoja na watendaji wa sekta ya ardhi wakati akiwa katika ziara ya siku moja kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi na kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi.

=Alisema ni vyema zoezi la kutambua wamiliki wa nyumba linalosimamiwa na TAMISEMI kupitia watendaji wake wa mitaa na vijiji likaenda sambamba na kutambua viwanja visivyolipiwa kodi pamoja na wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi kwa kuwa mazoezi hayo yana lengo la kuingizia serikali mapato.

="Hakuna maana kuchukua kodi ya jengo na kuacha kodi ya kiwanja, maana kodi zote hizo zina lengo la kukusanya mapato ya serikali yatakayosaidia katika kuendesha miradi mbalimbali ikiwamo ya kimkakati," alisema Dk. Mabula.

=Aidha, alizitaka halmashauri zote nchini kuhakikisha zinafikia asilimia 71 ya makusanyo ya kodi ya pango la ardhi kufikia mwezi ujao na kwa halmashauri itakayoshindwa kufikia kiwango hicho, wakuu wa idara au maofisa ardhi wateule watatakiwa kujitathmini kama wanaweza kuendelea na nyadhifa zao.

=Alisema, Mkoa wa Songwe uko nyuma katika makusanyo ya kodi ya pango la ardhi na kufikia Januari 2021 umekusanya asilimia 23 tu ya malengo kiwango alichokieleza kuwa ni kidogo na kuwaagiza wakurugenzi wa halmashauri katika mkoa huo, kuhakikisha wanasimamia idara za ardhi kwa lengo la kuongeza kasi ya makusanyo.

=Awali Mbunge wa Songwe, Philipo Mulugo, alisema kasi ndogo ya utoaji hati katika mkoa wa Songwe inachangiwa na watendaji wa sekta hiyo na kujitolea mfano yeye mwenyewe kuwa ilimchukua mitatu kufuatilia hati yake mpaka pale alipofikisha suala lake kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaz.

=Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwengela, alimweleza Mabula kuwa mkoa wake utaanza mara moja kuyafanyia kazi maagizo yake na kwa kuanzia, atataka kila mwezi katika kikao cha kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa taarifa za masuala ya ardhi.

# NMB kula faida na wateja wake

**Na Beatrice Moses**

BENKI ya NMB imesema itashirikiana na wateja wake kufaidi faida ya Sh. bilioni 250 iliyovuna mwaka jana.

NMB imepanga kugawa faida hizo kwa utaratibu maalum wa njia ya zawadi, jana, imezindua rasmi kampeni ya 'Bonge la Mpango' ambayo itawawezesha wateja wa benki hiyo kujishindia fedha taslimu na zawadi nyinginezo.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, akizungumza jana makao makuu ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam, alitaja faida hizo ni pamoja fedha taslimu Sh. 500,000, pikipiki ya miguu mtatu maarufu kama toyo.

Zawadi nyingine ni gari aina ya Tata ya kubebea mizigo maarufu 'Kirikuu' na gari la kifahari aina ya Toyota Fortuner yenye thamani ya Sh. milioni 169, ambayo itatolewa siku ya mwisho.

"Kampeni hii itakayodumu kwa miezi mitatu ni kama sehemu ya shukurani kwa wateja wetu baada ya mwaka jana, kupata faida ya zaidi ya Sh. bilioni 200 na kutangazwa na jarida la Global Finance kuwa sisi ndio benki salama zaidi katika ardhi ya Tanzania kuweka fedha," alisema Mponzi.

Alisema wateja wote wa benki hiyo wanaofikia milioni tatu wana nafasi ya kushiriki, ambapo watakaoshinda zawadi hizo watakabidhiwa kwa utaratibu uliowekwa.

"Katika kipindi chote cha kampeni hii, wateja wote wanaoweka akiba walau Sh. 100,000 wataingia kwenye droo ya wanaostahili zawadi zilizopo ambazo ni fedha taslimu shilingi 500,000 kwa washindi 10 kila wiki na zawadi nyingine, kulingana na utaratibu ulivyowekwa," alisema Mponzi.

Alisema, kampeni hii inalenga pia kwa wasio na akaunti za NMB kufungua akaunti ili wawe sehemu ya kampeni ili wapate zawadi kwa kuwa kila mmoja kwa sasa anaugulia maumivu ya msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka ulimaliza fedha.

Kwa upande wake Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema kampeni hii inahusisha wateja walio kwenye matawi nchi nzima, watahakikisha kila mshindi anapata zawadi yake kwa uhalali.



Makamu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Liwale Mjini, Mohamed Likoko akipanda mti juzi kwenye eneo la Shule ya Msingi Msufini, wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya mwasisi wa skauti duniani, Baden Powell, yaliyofikia kilele chake jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# 'Jitihada bado zahitajika ukatili dhidi ya watoto'

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), kimesema bado jitihada zinahitajika katika kupambana na vitendo vya ukatili kwa watoto.

Meneja Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini kutoka WLAC, Wigaya Kissandu, alisema kituo hicho kimeendelea kupokea kesi kuhusiana na matukio mbalimbali ya ukatili kwa watoto hao pamoja na kunyimwa haki zao za msingi.

Kissandu alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam katika mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyowashirikisha maofisa wa Jeshi la Polisi, Mahakimu, Ustawi wa Jamii, walimu na madaktari kutoka mkoa huo.

Alisema kwa mwaka jana pekee kituo hicho kilipokea kesi zaidi ya 400 zilizoripotiwa kwao zikiwamo za watoto kukosa matunzo na kutelekezwa na wazazi wao.

Alisema tatizo la baadhi ya wazazi kushindwa kuwajibika katika matunzo ya watoto wao ni miongoni mwa sababu zinazochangia wajiingize katika vitendo viovu na wengine kuishia mitaani.

Kissandu alisema watoto wana haki ya kulindwa ili watimize ndoto zao.

Pia alisema baadhi ya watoto waliofanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kushindwa kuendelea na masomo, vilisababishwa kwa kiwango kikubwa na baadhi ya wazazi kushindwa kuwajibika katika malezi yao.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Leah Mbunda, alisema matukio yanayoongoza kuripotiwa katika madawati ya jinsia katika kanda hiyo ni pamoja na ya malalamiko ya malezi kwa watoto hao, watoto kubakwa na kulawitiwa.

"Na ndio maana katika kuhakikisha ulinzi wa watoto, dawati huwa tunajitahidi kushughulikia makosa yote yanayohusiana na ukatili wanaofanyiwa watoto hao kwa haraka ili haki itendeke," alisema Mbunda.

Meneja Mahabusu ya Watoto, Daius Damas, alisema ili kukomesha vitendo vya ukatili kwa watoto, kila mtu ana wajibu wa kutoa taarifa kwa vyombo husika na kuwajibika katika kuwalinda.

# Malima aonya wasimamizi fedha za TASAF

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, amesema ofisi yake haitakuwa tayari kumfumbia macho msimamizi atakayekwenda kinyume cha malekezo ya serikali kuhusu utoaji wa fedha za kunusuru kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Malima alisema hayo, juzi mjini Musoma alipokuwa akizungumza na wana habari akitoa ufafanuzi wa fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mpango wa kunusuru kaya maskini mkoani mwake, ambao unatekelezwa na TASAF awamu ya tatu.

"Serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 37.55, kutekeleza shughuli za mpango wa kunusuru kaya maskini, ofisi yangu haitamfumbia macho msimamizi atakayekwenda kinyume cha malekezo ya serikali," alisema Malima.

Alisema, fedha hizo zilitolewa na serikali kuanzia Julai 2014 hadi Februari mwaka huu, na kwamba kaya 39,580 kutoka katika vijiji 354 ambazo zimenufaika na mpango huo.

"Katika kipindi cha Februari mwaka huu, halmashauri zote tisa zimepokea zaidi ya Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya malipo ya walengwa waliopo katika mpango huo, hivyo wasimamizi wahakikishe kila mlengwa anapa wa wanaufaika wote wanapata huduma za afya na ili kuwa na kizazi chenye maisha bora siku zijazo.

"Halmashauri ya Wilaya ya Butiama inaongoza kwa kuwa na kaya 6,342 zilizopo kwenye mpango huo ikifuatiwa na Rorya yenye kaya 6,246, Musoma vijijini yenye kaya 4,862 na Bunda vijijini ikiwa na kaya 3,657," alisema.

Alizitaja halmashauri nyingine ni Tarime Vijijini yenye kaya 3,333, Serengeti kaya 2,845, Manispaa ya Musoma kaya 1,964, Bunda Mjini 1,777 na Tarime Mji kaya 1,555.ta fedha kwa mujibu wa maelekezo ya serikali," alisema.

# Kasi watoto kukatisha masomo yamtisha RC

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amekerwa na kitendo cha wanafunzi zaidi ya 1,120 katika mkoa huo kubainika kusitisha masomo miaka minne iliyopita, huku Mamlaka ya Mji Mdogo Mikumi wilayani Kilosa ikiongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wa kike kupata mimba.

Ole Sanare alisema hayo wakati wa ziara yake katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi, ambapo alifanya kikao na wananchi wa kwa ajili ya kuweka mikakati ya ujenzi wa shule tatu za sekondari katika Tarafa ya Mikumi .

Sanare, alisema sababu ambazo zimechangia idadi kubwa ya wanafunzi kutoendelea na masomo na kupata mimba na kutembea umbali mrefu ili kufika shuleni ikiwemo ya Sekondari Mikumi, ambapo wanafunzi hulazimika kutembea zaidi ya kilometa 30 kila siku kufika shuleni.

Alisema hali hiyo imechangia wanafuzi kukaa katika nyumba za kupanga na wanafunzi wa kike wakijikuta wanashawishika kujiingiza katika mambo maovu, na kwamba kupata mimba kunatokana na kutokuwapo uangalizi wa karibu wa wazazi na walezi wao.

> **Hatua hiyo inasababisha wanafunzi wengi kupata changamoto nyingi ikiwamo wanafunzi wa kike kupata mimba na kupoteza haki zao za kupata elimu.**

Aliwataka wananchi katika maeneo ya shule ambazo wanafunzi wanasafiri umbali mrefu kwenda na kurudi shuleni kujenga hosteli ili wanafunzi hasa wa kike wakae shuleni ili kuwalinda na kutimiza ndoto zao wa kielimu.

"Hivi kama mzazi unaruhusu mwanao anakaa ghetto, unajuaje usalama wake, wazazi mnakuwa na amani na kulala salama, yaani mzazi unamuacha na kumpangishia chumba hapa, ikifika saa moja usiku naye anaenda kufanya shughuli zake," alisema Sanare.

Katika hatua nyingine, aliwataka watendaji wa vijiji Kata ya Mikumi kuwahamasisha wananchi kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo, huku akitoa onyo kali la kuwachukulia hatua za kisheria mwananchi ambaye atapingana na agizo la uchanga fedha kwa ajili ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa shule hizo.

Nao wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mikumi kwa kauli moja walikubaliana kujenga shule mpya tatu za sekondari zitakazoanza kutumika mwakani ili kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Mikumi ambayo ndiyo shule pekee kwenye mji huo.

Gladness Lukumayi, mkazi kijiji cha Ihombwe, alisema hatua hiyo ya kutaka kuenga shule mpya inatokana na wanafunzi walio wengi kutembea umbali mrefu kutoka wanakoishi hadi Shule ya Sekondari ya Mikumi.

Lukumayi, alisema hatua hiyo inasababisha wanafunzi wengi kupata changamoto nyingi ikiwamo wanafunzi wa kike kupata mimba na kupoteza haki zao za kupata elimu.

Naye Elius Edward, Mkazi wa kijiji cha Msimba, alisema changamoto wanazokumbana nazo wazazi katika kuwasomesha wanafunzi hao ndizo zinazosababisha wananchi kuwa na hamasa ya kujenga shule katika kijiji chao ili kuepukana na gharama za kuwalipia usafiri watoto wao kila siku.



Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serera (kushoto), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Mumi iliyopo Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma jana, alipotembelea shule hiyo kukagua maendeleo ya elimu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wataalamu waelekezwa usimamizi vyanzo mapato

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya Mkuranga mkoani Pwani, Mohamed Mwera, amewataka wataalamu wa Halmashauri hiyo, kusimamia miradi ya maendeleo, ikiwamo vyanzo vya mapato.

Hayo yalisemwa na Mwela, katika kikao maalumu Cha baraza la madiwani wa Halmashauri hiyo.

" Ni jukumu la wataalamu kusimamia miradi ya maendeleo, vikiwamo vyanzo vya ndani vya mapato ili viweze kuleta maendeleo katika halmashauri," alisema.

Alisema atakayeshindwa kusimamia miradi ya maendeleo na kuwakosesha wananchi maendeleo, atachukuliwa hatua.

Wakati huohuo, madiwani wa Halmashauri hiyo, wamepitisha bajeti ya Halmashauri yenye jumla ya Sh. bilioni 49.7 zikiwemo Sh. bilioni 7.8 zinazotarajiwa kukusanywa kupitia mapato ya ndani ili kutekeleza miradi ya maendeleo sekta mbalimbali kwa mwaka 2021-22.

Ofisa Mipango wa Halmshauri ya Wilaya hiyo, Kaunga Amani, alitaja vipaumbele vya bajeti hiyo ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi (CCM) ya mwaka 2020-25, sera ya Taifa na maelekezo ya Serikali kupitia Waziri wa (TAMISEMI), Selemani Jafo.

# Watakiwa kuanza biashara saa 12

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, ametoa agizo kwa wafanyabiashara wa matunda eneo la Mailimoja kuanza biashara saa 12, jioni na atakayekiuka hatua zichukuliwa dhidi yake.

Ndikilo alitoa agizo hilo juzi alipozungumza na wafanyabiashara wa soko la Loliondo na soko jipya la Picha ya Ndege kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao katika eneo la Mailimoja wanatakiwa kuanza saa 12 na muda mwingine waendelee katika soko la Loliondo.

**Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya mtende haki, anayetaka kufanya boashara ya matunda aanze saa 12 na si saa saba.**

"Mkurugenzi, Mkuu wa Wilaya mtende haki, anayetaka kufanya boashara ya matunda aanze saa 12 na si saa saba kama ilivyo sasa atakayekiuka mgambo kamata," alisisitiza Ndikilo.

Kuhusiana na gharama za kodi zinazotozwa kwa skwea mita, alimuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji kukaa na uongozi wa wafanyabiashara hao kujadiliana namna ya kutatua kero zinazowabili. Awali aliwasilisha kero za wafanyabiashara wa Loliondo Mwenyekiti wa soko hilo, Mohamed Mnembwe, aliomba kupunguzwa kwa gharama za kodi kwa mwezi ambazo wanatakiwa kutoa Sh. 8,000 ifike Sh. 3,000 ambayo wanna uwezo wa kuimudu.

Aidha, Mnembwe alisema uwapo wa kodi kubwa ya Sh. 8,000 imesababisha baadhi ya fremu kutotumika, na kwamba kati ya wafanyabiashara zaidi ya 338, ni 88 pekee wanaoendelea na biashara na zaidi ya 200 wamefunga fremu kwa kushindwa kulipia kodi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Jenifa Omolo, alisema suala hilo la kuomba kushushiwa kodi hadi Sh. 3,000 halikuwahi kumfikia ofisini kwake, na kwamba yuko tayari kukaa meza moja na uongozi wa soko kujadili kodi rafiki.

Solo la Loliondo lilianzishwa baada ya kuvunjwa kwa soko la Mailimoja ambalo lilikuwa kwenye hifadhi ya barabara, wafanyabiashara waligawiwa maeneo na kila mmoja alijenga kwa gharama zake kwa makubaliano na Halmashauri.

Kodi ya awali ilikuwa Sh.11, 000, lakini baada ya majadiliano ilishuka hadi Sh. 8,000, ingawa nayo inaelezwa kuwa kikwazo kwa baadhi ya wafanyabiashara kuendelea na biashara zao.



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Nyabaengere, Kata ya Musanja, Wilaya Musoma mkoani Mara, wakisomba mawe juzi, kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho ili kuwaondolea usumbufu wa kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Daraja kuziunganisha Misungwi, Nyamagana

**Na Erick Mwanakulya,** MWANZA

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), mkoani Mwanza umedhamiria kuunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana kupitia ujenzi wa daraja la Mwasongwe lililopo Mto Nyashishi ili kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za usafiri na usafirishaji kwa urahisi.

Hayo yalisemwa na Meneja wa TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, Mhandisi Alzabron Kayungi, katika mahojiano maalum kuhusu maendeleo ya ujenzi wa daraja hilo lililopo katika Barabara ya Kaluluma-Mwasonge-Nyashishi yenye urefu wa Km 7 iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na Barabara ya Buhongwa-Mwasongwe yenye urefu wa Km 4 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana.

"Daraja hili la Mwasonge lililopo Mto Nyashishi lina urefu wa Meta 60 na limefikia asilimia 65 kukamilika na litagharimu Sh. bilioni 1.78, daraja hili linaunganisha Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi na litakamilika mwanzoni wa mwezi Mei mwaka 2021," alisema Mhandisi Kayungi.

Mhandisi Kayungi aliongeza kuwa wakazi wa Kijiji cha Mwasongwe kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi wanategemea daraja hilo ili kupata mahitaji yao kama shule, hospitali na huduma nyingine za kijamii, huku wakazi wa Nyamagana wanategemea malighafi za ujenzi kama mawe, mchanga, kokoto kutoka katika Kijiji cha Mwasongwe, hivyo uwapo wa daraja hilo utasaidia wananchi kufanya shughuli zao za kila siku kwa urahisi.

Msani Said Faida, mkazi wa Kigongo Ferry, ameipongeza Serikali kupitia TARURA kwa Ujenzi wa daraja hilo kwani litawasaidia kufanikisha kupata huduma zao za kijamii kama shule, hospitali pamoja na huduma ya masoko katika soko la Buhongwa.

Alisema kuwa daraja lililopo kwa sasa ni la miti ambalo pia ni hatarishi kwa usalama wao katika kusafirisha bidhaa, pia katika kipindi cha masika wanatumia mtumbwi kuvuka ambapo si salama, hali inayopelekea kukwamisha shughuli zao na kusababisha kuzunguka umbali mrefu kwa kupitia usagara ili kuzifikia huduma mbalimbali.

"Naishukuru sana Serikali kupitia TARURA, kwa ujenzi wa daraja hili la Mwasongwe na kutusaidia kufika Buhongwa kwa urahisi, tulikuwa tunateseka katika uvukaji kwa kutumia daraja hili la miti na kipindi cha masika tulikuwa tunatumia mitumbwi kuvuka ambapo haikuwa salama kwetu," alisema Msani Faida.

Meneja wa TARURA Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana, Mhandisi Mohamed Muanda, alisema kuwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana wapo katika ujenzi wa Daraja la Fumagila lenye urefu wa Meta 30, lililopo katika Mto Nyashishi Kata ya Kishiri linalounganisha Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana, Halmashauri ya Wilaya Misungwi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Magu ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 95 na kugharimu Sh.milioni 552 mpaka kukamilika.

"Daraja hili la Fumagila lililopo katika Mto Nyashishi katika barabara ya Kishiri - Fumagila limefikia asilimia 95, na ni muhimu kwa wakazi wa maeneo haya kwani kipindi cha masika ilikuwa tabu kuvuka, pia wakazi wa Magu, Misungwi wanategemea kupata huduma katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana Kata ya Kishiri, daraja hili ni mkombozi kwa wakazi wa maeneo haya kwa kuwa wanategemeana sana," alisema Mhandisi Muanda.

Aidha, mbali na ujenzi wa Daraja la Fumagila na Mwasongwe, Mratibu wa TARURA Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Gaston Gasana, alisema kwa kutumia malighafi za ujenzi kama mawe zilizopo kwa wingi mkoani Mwanza, wameweza kujenga barabara za mawe maeneo ya milimani zenye urefu wa Km 11 kwa gharama nafuu.

## Sababu kukwama ujenzi ofisi ya h/shauri hizi

**Na Samson Chacha,** TARIME

UJENZI wa jengo la ofisi ya makao makuu ya Halmashauri ya mji Tarime umekwama, kutokana na mkandarasi kudai kuchelewa kwa vifaa vya ujenzi.

Sababu nyingine ni ucheleweshaji wa malipo kutoka Serikali Kuu na uzalishaji duni kutoka katika viwanda vya Dar e Salaam ambako amenunua vifaa hivyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Daniel Komote, amesema ujenzi huo umekwama kwa zaidi ya miezi nane sasa na kuahidi Halmashauri kufatilia mradi huo kwa karibu ili uweze kukamilika.

Alisema kwamba mkandarasi alishapokea Sh. 1.538, 932,264.21 kati ya Sh. 3,115,458,992.30.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, mwenyekiti huyo alisema:" Halmashauri yetu ya Tarime Mjini iliingia mkataba wa ujenzi wa jengo mpya la ofisi za utawala lililopo eneo la Bomani na Mkandarasi Tanzania Building Agency ( TBA ) tulikubaliana mkataba tangu 2017 na ulianza kutekelezwa kuanzia Aprili 26, 2018 na ulitarajiwa kukamilika Januari 31, 2021, lakini mradi huo umekwama kuendelea mbali na kuwa kwenye hatua ya upauaji ukiwa kwenye asilimia 66... mkandarasi alishalipwa Sh. 1,538,932,264.21 sawa na asilimia 49.4, huku mkandarasi akiomba kuongezewa mda wa siku 365 kuanzia Februari 2 , 2021 ambapo maombi yake hayo hayajajibiwa ."

Nipashe
TESA
Jumanne Februari 23, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 12

## Wadau ndiyo maelekezo ya wanafunzi kumaliza ukeketaji



Ukurasa 13

## Bajaji, bodaboda zisigeuke 'wahalifu' wanaokubalika

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA MWAKANGALE

AUGUST MBUYA

# Mbunifu tanuri rafiki la 'taka za hedhi'

## •Mlinzi heshima mwanamke , mazingira

WASICHANA na wanawake bila kujali wanapoishi iwe mjini au vijijini wanahitaji pedi, maji, faragha ya kujisitiri wakati wa hedhi pamoja na sehemu ya kuhifadhi taulo walizotumia ili zisichafue mazingira pamoja na kuwadhalilisha.

Katika maeneo tofauti ikiwamo vyuo, taasisi na baadhi ya shule za msingi au sekondari hakuna vyombo vya kuhifadhia pedi zilizotumika na utaratibu bora wa kuziteketeza pia ni changamoto.

Aidha, hedhi salama inatatizwa na ukosefu wa maji shuleni, vyuoni na katika vituo vya afya na zahanati na hiyo ni changamoto inayosababisha wanafunzi wasichana kukosa masomo kati ya siku 40 hadi 50 kwa mwaka (vyuoni na shuleni).

August Mbuya (pichani), mhandisi wa rasilimali maji na umwagiliaji kutoka Chuo cha Maji, jijini Dar es Salaam, anasema amezitazama changamoto za wanawake na sasa ana jibu la kuwasaidia kwenye eneo la kuhifadhi taulo zinazotumiwa wakati wa hedhi na kuziteketeza.



Anasema katika masomo yake ameangalia namna bora ya kulinda utu wa mwanamke, akisema:"Mimi ni mwanaume lakini nikaamua kuja na suluhisho la masuala ya wanawake, wakati nikiwa mwaka wanne chuoni nilibuni banda salama kulinda utu wao."

"Nimesoma Sekondari ya Old Moshi ambayo ni ya wavulana. Tulikuwa na utaratibu wa kutembeleana shule kwa shule hasa kidato cha tano na sita. Nilipotembelea shule za wasichana muda mwingi nilifanya tathmini nikipendelea kufuatilia masuala yao kujua namna watakavyosaidiwa ili kuongeza ubora kwenye masomo yao."

Mbuya (25) akizungumza na NIPASHE hivi karibuni, Dar es Salaam, anaeleza kuwa kwa msingi huo alibuni mambo ya kuwasaidia wanawake kwa kutumia ubunifu na utafiti.

"Changamoto zao kubwa nilipozungumza na wasichana ilikuwa ni vyoo na namna bora ya kuhifadhi na kuharibu taka au taulo za hedhi. Nikawa natamani kupata ufumbuzi ni namna gani naweza kubuni mazingira ya kuwasaidia."

"Nikabaini kuwa katika siku zao za hedhi ambazo ni kati ya tatu na tano wengine wanakumbana na changamoto zikiwamo za mazingira.

Mwingine anakuwa katika siku zake kipindi cha mtihani wa taifa, mitihani ya kawaida, au vipindi vya darasani, hayo matukio yote yakanifanya niwe mdadisi," anasema Mbuya.

### VYOO KUZIBA

Anakumbusha kuwa kuna wakati walizungumzia kuhusu vyoo kuziba kila wakati na katika mazungumzo hayo walimwelezea kuwa vinaziba mara kwa mara na kuona kuwa ilikuwa kero kubwa kwao.

Anasema alipofanya maombi ya chuo kikuu alivutiwa na kusoma masuala ya maji na lakini wazo la kubuni mbinu ya kuboresha mazingira ya vyoo kuziba kutokana na kukosa sehemu ya kuhifadhi pedi na badala yake kuzirusha vyooni likapotea katika fikra.

"Ila mwaka wa tatu lilinijia tena na nilipotembelea shule ya Kibasila ya Dar es Salaam, hospitalini na taasisi zenye mikusanyiko baadhi changamoto nilizikuta ni hizo hizo," anasema Mbuya.

Kutatua kero hiyo Mbuya anasema alibuni 'incinerator' au tanuru linalojengwa kwa matofali ambayo hutumika kuchomea taka akilenga taulo za hedhi," anasema Mbuya.

"Asilimia 40 hadi 60 ya vitu au taka zinazofanya mfumo wa maji taka kuziba, inatokana utupwaji wa pedi katika vyoo," anasema.

### KUTUMIA BANDA SALAMA

Mbuya anasema amefanya utafiti miundombinu ya majitaka iliyopo Dar es Salaam amebaini hilo na kwamba , utupaji wa pedi chooni si jambo jema wala kuzifukia ardhini kote kunachafua mazingira," anaeleza Mbuya.

"Iwapo mwanamke akitumia pedi za kila mwezi hadi kumaliza nimebaini zina uzito takriban gramu 300 na hata nusu kilo."

Anaongeza:"Kwa mfano chuo kina wanafunzi wa kike 1,000 ukizidisha kwa gramu 300 kila mwezi wanazalisha kilo 300,000 za pedi sawa na tani 300. Na Tanzania bado hatuna mfumo wa kurejeleza (recycling) pedi, hizi kilo ni nyingi, ndiyo sababu ya kubuni banda salama."

### UFUMBUZI

Injinia Mbuya anasema kuliko na kundi kubwa la wanafunzi kama mabwenini kuna kilo nyingi za pedi zinazotumika na utupaji wake unaweza usitunze utu wa mwanamke iwapo zitazagaa ovyo jalalani bila kuteketezwa.

Anasema hata kutupwa kwa kuchanganya na taka nyingine katika vyombo vya kuhifadhia taka si sahihi kwa kuwa haziozi.

Pia anaeleza ilivyo tatizo kwa wahudumu wa usafi kwenye maeneo ya shule hizo au taasisi, kwa kuwa taulo nyingine zinaanza kuoza na iwapo gari la kubebea taka halijafika kuzizoa kwa wakati sehemu zinapohifadhiwa kunanuka.

"Kwanza wahudumu hawapo katika maeneo ya shule za umma iwe sekondari au msingi, labda shule binafsi, lakini nao wanakumbwa na changamoto kwani vyombo vya kuhifadhia pedi vikijaa hawana pa kuzipeleka hadi gari la taka litakapofika baada ya siku tatu au wiki."

Anasema linahitajika eneo ili kutupa taka za hedhi mara tu chombo kinapojaa na kupunguza harufu chooni.

Utamaduni wa kila mwanamke alivyofundishwa, ni kuhifadhi ipasavyo mahali sahihi taka hizo baada ya kuzitumia, aidha kwa kuchoma ili mwingine asione.

Anaeleza kuwa ndiyo maana wanapokuta chombo kimejaa wanazitumbukiza chooni mwishowe kinaziba, lakini wapo wanaozifukia hasa kwenye eneo binafsi, kwa wanafunzi si rahisi, hata kuchoma wanahitajika kuni.

Katika utafiti alioufanya tangu akiwa shule hadi chuo, alipohitimu aliamua kuja na suluhisho la kuwa na eneo la kuteketeza pedi, aliloliita banda salama.

Anasema wazo hilo alilipata akiwa kwenye mafunzo ya vitendo ambayo mwanachuo analazimika kuyafanya.

"Mwanzo nilikuja na majina tofauti, niliamua kusema banda salama ili kulinda utu wa mwanamke, kwa hiyo nikaamua kuwa na jina rahisi ili kukubalika katika eneo lolote."

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Wadau ndiyo maelekezo ya wanafunzi kumaliza ukeketaji

SHERIA ya Mtoto ya 2009 inasisitiza kumlinda mtu wa chini ya miaka 18 na ibara 13(1) inaeleza haya:" Ni kosa la jinai kumsababishia mtoto mateso au adhabu za kikatili, matendo yasiyo ya kibidamu au vitendo vya kumdhalilisha ambavyo ni pamoja na mazoea ya tamaduni ambazo hazina utu au zinasababisha maumivu kimwili na kiakili kwa mtoto".

Licha ya kuwapo sheria hiyo ukeketaji unaosababisha mateso kwa mabinti na wanawake ambao unakwenda kinyume na matakwa ya sheria unaendelea pamoja na kufanyika uhamasishaji wa kupinga mila hiyo iliyopitwa na wakati.

Februari 6 mwaka huu, ilikuwa ni kilele cha maadhimisho ya siku ya kimataifa ya Kupinga Ukeketaji ikiwa na kaulimbiu "Hakuna muda wa kutochukua hatua. Ungana, fadhili na chukua hatua kukomesha ukeketaji".

Maadhimisho ya siku hiyo hulenga kuhimiza serikali, asasi za kiraia, mashirika na jamii kuongeza uelewa na kutokomeza ukeketaji, ambao unaathiri wanawake na wasichana kote duniani.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, baadhi ya wanafunzi wa Dar es Salaam, wanaomba wigo upanuliwe zaidi kwenye utoaji wa elimu ya kupinga ukatili huo ili wengi wajitambue na wawe tayari kuukwepa.

Wanatoa wito huo katika kampeni za kupinga ukeketaji zilizofanyika kwenye kata za Kivule na Kitunda, zikihusisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, serikali na wasaidizi wa kisheria.

Washiriki wengine katika kampeni hizo ni wa vituo vya taarifa na maarifa na Mpango wa Taifa wa Kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), ngazi ya kata.

Mmoja wa wanafunzi hao, Asia Salum wa Sekondari ya Kivule , anasema, tatizo la ukeketaji ni mtambuka linaathiri mamilioni ya wanawake na wasichana kote duniani, hivyo elimu ya kulikabili inatakiwa kupanuliwa zaidi.



Baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari zilizopo Kivule jijini Dar es Salaam, wakiwa na mabango yenye ujumbe wa kupinga ukeketaji. **PICHA: SABATO KASIKA**

### NINI KIFANYIKE?

Anasema, ukeketaji ni mkubwa, lakini anaamini ni wanafunzi wachache wanaojua madhara ya ukeketaji, hasa wa mijini na kwamba ipo haja elimu hiyo kutolewa zaidi kwenye maeneo ambayo mila hizo zinafanyika.

"Wadau wa kupinga ukeketaji wanaweza kuwa na ratiba ya vipindi ya kutoa elimu hiyo katika shule zote za vijijini hasa kwenye mikoa ambayo yanasifika kwa ukeketaji ili kukomesha vitendo hivyo," anasema Asia.

Mwanafunzi huyo anafafanua kuwa elimu hiyo isiishie shuleni bali hata wazazi, walezi, ngariba na wazee wa kimila nao waelimishwe vya kutosha, kwa maelezo kwamba hao ndiyo tatizo.

Pili Makulu wa Shule ya Sekondari Abuu Juma, anasema, maeneo ya Kivule yamekuwa yakitajwa kuwa na vitendo vya ukeketaji, hivyo wanafunzi wa shule zote za maeneo hayo wafuatiliwe na kupewa elimu.

"Huwa ninasikia kwamba huku Kivule kuna watu kutoka mikoa inayokeketa na yanaendelea kufanya vitendo hivyo, ninawashauri nyie watoa elimu mje huku shule kwetu mfundishe madhara ya ukeketaji," anasema Pili.

Anasema, wanafunzi wakipewa elimu ya kutosha kuhusu madhara ya ukeketaji, wataifikisha kwa wazazi wao na kwamba kwa utaratibu huo, kuna uwezakano wa kumaliza vitendo hivyo kwenye jamii.

"Ninaamini kwamba, kampeni ya kupinga ukeketaji na jitihada za pamoja vinahitajika kwa ajili ya kumaliza tatizo hili. Kikubwa zaidi wadau kuanzisha ratiba ya kutoa elimu katika shule mbalimbali na kuwafikia wale wote wanaohusika na kuendeleza mila hii potofu," anasema.

Anasema, vita dhidi ya ukeketaji isisubiri siku ya maadhimisho tu bali mikakati ya kupanua wigo wa utoaji elimu ya kupinga vitendo hivyo inahitajika ili kumwezesha mtoto wa kike kusoma bila hofu ya kukatisha masomo.

### KUPENDA UHALIFU

Viongozi wa dini waliokuwa kwenye kampeni hizo, wanasema umefika wakati jamii kuachana kukumbatia mila ambazo zinakwenda kinyume na kile ambacho Mwenyezi Mungu ameagiza.

Mchungaji Joseph Mapunda wa Kanisa la Calvary Assembulies of God (ACG) la Kivule Machimbo, anasema, katika maandiko matakatifu, hakuna sehemu inayohalalisha ukeketaji.

"Ukeketaji ni kwenda kinyume na kile ambacho Mungu ameagiza, kwani wanaume ndiyo wameruhusiwa kutahiriwa, siyo kukeketa wanawake, hivyo wanaokeketa wanamkosea Mungu," anasema Mchungaji Mapunda.

Abdi Mahanyu ni Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Kipunguni, anasema, ukeketaji ni kumkosoa Mungu, na kwamba wanaofanya hivyo, wanapingana na uumbaji wake na kufuata matakwa yao wenyewe.

Mzee wa kimila wa eneo la Kivule, Joseph Gasaya, anasema dunia ya leo imebadilika, na kwamba wanaoendekeza mila za ukeketaji hawana budi kubadilika na kuachana nazo.

"Ukeketaji ulikuwa enzi hizo wakati sisi tungali vijana huko nyumbani kwetu Musoma, lakini dunia imebadilika, magonjwa yameongezeka, hivyo niwaombe wanaoendelea kukeketa waache," anasema Gasaya.

### NI VITA YA JAMII

Mratibu wa Miradi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambao waliratibu kampeni hizo, Hellen Urio, anasema kila mtu akishiriki katika vita ya kukomesha vitendo vya ukeketaji nchini.

"Jamii inatakiwa kutambua kuwa vita dhidi ya ukeketaji ni ya kila mtu katika eneo lake. Kila mmoja akishiriki, vitendo vya ukatili ukiwamo huo wa ukeketaji, vitakoma nchini, hivyo tuendelee kushirikiana," anasema Urio.

Urio anasema, wanafunzi ni miongoni mwa waathirika wakubwa wa ukeketaji, na kuwaelekeza kuwa wanapoona dalili au tukio la ukeketaji, watoe taarifa haraka ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

"Kuna sehemu nyingi za kutoa taarifa kuanzia vituo vya taarifa na maarifa, MTAKUWWA, kwa wasaidizi wa kisheria na hata kwenye madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya polisi," anasema.

Mratibu huyo anamtaka kila mtu mwenye taarifa yoyote ya vitendo hivyo kuifikia mahali husika, na kwamba kufanya hivyo ni moja ya elimu ya kupambana na ukeketaji kwenye jamii.

# Mbunifu tanuri rafiki la 'taka za hedhi'

INATOKA UK.11

BANDA RAFIKI

Mbuya anasema banda hilo ni rafiki wa mazingira kwa kuwa chanzo cha nishati ya kuteketeza pedi hizo ni gesi ya kinyesi inayotoka kwenye vyoo vya shule au taasisi iwe hospitali au chuo.

Mbunifu huyo anasema iwapo hakutakuwa na usimamizi makini banda hilo linaweza kuwa na madhara kwa muda mrefu lakini atatoa mwongozo kulisimamia.

"Banda hilo litazalisha mbolea maana baada ya taka hizo kuchomwa majivu yanaweza kutumiwa kupanda mazao kama mboga bustanini." Anasema.

### MATARAJIO

Mbuya ambaye mwishoni mwa mwaka jana jijini Dodoma alipokea tuzo ya ubunifu wa wazo hilo aliloliwasilisha mbele ya wadau wa maji ikiwamo wizara, baada ya mchakato wa kupatikana washindi wa ubunifu, alipata tuzo ya ubunifu.

Anasema tuzo hiyo alipewa na Association of Tanzania Water Suppliers (ATAWAS) ambao huandaa mkutano wa wadau wa maji kitaifa.

Pamoja na kuwapo kwa changamoto ya ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu, Mbuya anasema baaada ya kuhitimu masomo yake kwa miaka minne chuo cha maji, anafikia kuanzisha taasisi yake na kuajiri.

"Nikiwa chuo nilipata ushirikiano mdogo kutoka kwa wenzangu kuhusu wazo hili, walinicheka na kuniita 'jamaa wa pedi' sikuchukuliwa kama changamoto.

Watu wamezoea kuwa na 'mawazo ambayo ni ya kawaida. Tukiwa vyuoni, nikaamua kuja na suluhisho kwa wasichana katika kukabiliana na changamoto za hedhi na kulinda utu wao, hata kulinda mazingira," anasema Mbuya.

Anaeleza kuwa kampeni za kugawa pedi bure kwa wanafunzi, anaziunga mkono ingawa kunahitajika vitu vingine kwenda sambamba ikiwamo namna ya kuzitupa.

Mbuya anashauri Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTEC), kuweka wataalamu wake vyuoni ili kushirikiana na wabunifu kuboresha na kusaidia utekelezaji wa mawazo wa wanachuo vyuoni.

"COSTEC ikiwa vyuoni ni rahisi kuliendeleza wazo, badala ya kusubiri nihitimu hadi kuja kuwasilisha wazo nikipata shughuli za kiuchumi siwezi kulifanyia kazi nitakosa muda," anasema Mbuya.

MAKALA
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Bajaji, bodaboda zisigeuke 'wahalifu' wanaokubalika

UKITEMBEA kwenye njia za waenda kwa miguu za majiji na miji mikubwa unaweza kuchanganyikiwa. Unakutana na mboga, mitumba, matunda, viatu na bidhaa nyingine lukuki, hivyo kukosa pa kupita.

Pamoja na bidhaa zilizotandazwa chini ngoma za masikio huumizwa na kelele za kila namna, za wamachinga, za vipaza sauti zilizorekodiwa kutoa matangazo ya kuita wateja na nyingine ni za vyombo vya moto zikiwamo honi na mingurumo.

Unaweza kuchanganyikiwa kwa sababu njia na madaraja ya kutembea zimevamiwa na wamachinga na kuwaweka watumiaji kwenye hatari ya kuumizwa na vyombo vya usafiri.

Pamoja na bidhaa na kelele za kuita wateja, kero nyingine ambayo huambatana na hiyo ni uegeshaji wa bajaji ovyo barabarani.

Hilo hufanyika sehemu nyingi za mijini kiasi cha wakati mwingine watu kuwaza hivi inakuwaje, kwenye mizunguko wa barabara kunajaa bajaji wakati kuna walinda usalama pamoja na wadhibiti usafirishaji ardhini?

Huu unaweza kuchukuliwa kama uvunjaji wa sheria za barabarani wa makusudi unaosababisha kila mahali kuwa eneo la kuegesha bajaji na pikipiki.

Imezoeleka kuwa mara nyingi sheria za barabarani zinapovunjwa, wanaochukuliwa hatua kwa wepesi ni madereva wa magari, lakini kinachoonekana sasa wanaoongoza kuvunja sheria hizo ni bodaboda na bajaji.

Madereva hao wamekuwa wakisababisha ajali za mara kwa mara kwa sababu ya kutozingatia sheria na alama za barabarani. Bajaji huegeshwa kila mahali iwe kwenye kona , mizunguko ya barabara na popote pale wanapopata vijiwe.

Mathalani eneo la Njianne kwenye barabara ya Goba-Mbezi jijini Dar es Salaam ni kituo cha bajaji lakini cha kushangaza kipo kwenye mzunguko wa barabara ambao unaelekea Madale , Mbezi, Kimara na Goba.

Eneo hilo si salama kwa abiria maana kwenye mzunguko huo lolote linaweza kutokea kutokana na kukurukakara zinazohusisha magari yanayoelekea kwenye pande zote nne za barabara.

Madereva wa bajaji wamezoea kuachwa kuendelea na mwenendo huo na wanajiona kuwa wanachofanya ni halali.

Kwenye hali kama hiyo madereva wa babaji wataendelea kuumiza watu kwani hawana hofu ya kuegesha wao hujiwekea 'chimbo' popote wanapotaka ili mradi manispaa itakusanya kodi.

Bajaji ni usafirishaji ambao mara nyingi umejaa vurumai, kelele na hata kukamiana kunakoongeza vurumai na tafrani bila sababu. Tofauti na madereva wa magari, wanaoendesha bajaji mara nyingi hawana hofu, kwa vile wanafahamu waathirika wakubwa wa kupigwa faini ni wale wanaoendesha magari.

Bodaboda na bajaji hawana hofu hufanya watakalo, wapo wasiojali taa wala askari wa usalama barabarani na huamua wakati mwingine watakalo.

Ni kawaida kuonekana wakichomoka na kupita kwenye makutano ya barabara bila kujali uwepo wa waongoza magari. Wanahisi boda boda hazihitaji kuruhusiwa, cha msingi ni upenyo na hujiamini kuwa ni wazoefu na wabobezi kuvunja sheria.

Tabia hii ya kuchomoka kama wanavyotaka imewapa ubabe, kiburi na jeuri ya kudharau madereva wengine licha ya kusababisha uharibifu wa vyombo vyao, hawajali badala yake wanaposababisha ajali hukimbia na kuingia mitini.

Licha ya kwamba bajaji hazijaweza kuchomoka kama bodaboda lakini pia madereva wake wana kero nyingi hasa uegeshaji mbovu, usiodhibitiwa.

Kuna madai kuwa magari ya mwendokasi hayana msamaha na pikipiki wala bajaji na inapotokea zinaingia kwenye njia yake ni kwa nadra abiria wakanusurika.



Bajaji na pikipiki ni usafiri muhimu lakini kama hautadhibitiwa unakuwa kero. **PICHA: MTANDAO.**

> Eneo hilo si salama kwa abiria maana kwenye mzunguko huo lolote linaweza kutokea kutokana na kukurukakara zinazohusisha magari yanayoelekea kwenye pande zote nne za barabara.

**UFUMBUZI**

Kwa Dar es Salaam na miji mikubwa kuna eneo kubwa la hifadhi ya barabara , halmashauri zijielekeze kuweka miundombinu kwenye maeneo hayo ili kuwa na 'stendi' au vituo rasmi vya bajaji na pikipiki.

Maofisa usalama, wahandisi wa miji na wataalamu wa kudhibiti usafiri wa ardhini wasaidie kufanikisha hilo kwa sababu ni kero na mara nyingine haivumiliki.

Jeshi la Polisi linasema kwa mwaka jana 2020 watu 1,158 walipoteza maisha wakati 2,089 walijeruhiwa kati ya Januari hadi Novemba mwaka huo, kutokana na ajali za barabarani.

Polisi wanatangaza kuwa kiwango cha ajali za barabarani kwa mwaka jana kilipungua kwa asilimia 33.9 kikilinganishwa na mwaka 2019, ripoti hiyo inayotolewa na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi Liberatus Sabas, inasema, kati ya Januari hadi Novemba 2019 zilitokea ajali 2,722 na kati ya hizo zilizosababisha vifo ni 1117 na waliopoteza maisha ni 1,329.

Jeshi la Polisi ni mahiri kutoa takwimu hizo lakini pia ni vyema liende mbali na kuchambua visababishi na kuvitafutia dawa hasa ajali zinazohusisha kujiamulia mambo kama ilivyo kwa bodaboda na bajaji.

Mbali na hilo ni vyema kusikia jinsia polisi ilivyokabiliana na wanaotumia simu barabarani ambao nao ni chanzo cha ajali.

Wakati mwingine kutumia simu barabarani ikiwa ni pamoja na kuweka foni masikioni kumekuwa chanzo cha ajali hasa kwa waendesha pikipiki na bodaboda ambao wanapotumia vifaa hivyo hawasikii honi wala milio ya magari yaliyo nyuma yao.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, KAHAMA

# TASAF yawanusuru waliokata tamaa kuendelea na masomo



Faida Joseph wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Wichamike, akielezea namna mfuko wa maendeleo ya jamii ulivyomnusuru kielimu baada ya wazazi kukosa fedha za kumtimizia mahitaji. **PICHA: MARCO MADUHU**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini, ulioanza mwaka 2002, una mengi ya kujivunia ikiwamo kusaidia watoto wengi kusoma.

Mwaka 2015 serikali ilitangaza kutoa elimu bure kuanzia wanafunzi wa shule za awali hadi sekondari kwa lengo la kusaidia kupata elimu bila ya kujali hali za uchumi wa familia zao.

Licha ya serikali kugharamia elimu zipo baadhi ya kaya zinashindwa kuwapeleka watoto shule kutokana na ukosefu wa fedha za kumudu mahitaji kama sare, daftari, kalamu na chakula.

Kupitia ruzuku yenye masharti fedha hizo zitumike kupeleka watoto shule na kuwanunulia mahitaji, hali hiyo ilianza kurudisha matumaini ya wanafunzi waliokata tamaa na shule kuendelea na masomo.

Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, ni miongoni mwa maeneo ambayo shule za msingi zilikuwa na tatizo la wanafunzi wanaotoka kwenye kaya maskini kuwa watoro shuleni na wengine kuacha masomo.

Sababu ya changamoto hiyo inatajwa kuwa ni kukosa mahitaji muhimu ya shule na kwamba TASAF kuwa mkombozi.

Modesta Alphonce ni miongoni mwa watoto ambao wazazi wao ni wanufaika TASAF, anayesoma darasa saba katika Shule ya Msingi Wichamike, iliyoko Kijiji cha Ntobo.

Anasema kabla ya wazazi wake kuingia TASAF, alikuwa mtoro shuleni sababu ya kukosa mahitaji muhimu kama sare na daftari.

Anasema baada ya kukosa mahitaji hayo alijiingaza kwenye kazi za kulima vibarua kwenye mashamba ya watu binafsi na wazazi wake, ili wapate fedha ya chakula, pamoja na na mahitaji mengine.

"Nilikuwa nimeshakata tamaa kusoma, kutokana na nyumbani kwetu kuwa maskini, na kushindwa kunitimizia mahitaji ya shule, sababu huwezi kwenda shule bila ya kuvaa sare, viatu wala kuwa na daftari, na ukizingatia mimi ni mtoto wa kike bado na mahitaji mengine yalikuwa yananisuburi " anasema Modesta.

"Baada ya wazazi wangu kuingia kwenye mpango wa TASAF, maisha yalibadilika na sikuweza tena kuwa mtoro shuleni. Ufaulu umeongezeka sababu sikosi masomo tena. Nimetoka kushika nafasi ya 40 na sasa nashika ya 10," anaongeza Modesta.

Mwanafunzi Faida Joseph, anayesoma darasa la saba katika shule ya Wichamike, anasimulia kuwa baada ya kukosa mahitaji hayo muhimu ya shule, alikata tamaa na masomo na kwenda kuchunga mifugo.

"Tangu nikiwa darasa la kwanza nimesoma kwa shida kutokana na wazazi wangu kuwa maskini na kushindwa kuninunulia mahitaji ya shule kama sare, viatu, madaftari, na baada ya kufika darasa la nne nikaona maisha ya shule ni magumu ikabidi nianze kuwa mtoro," anasema Sahani.

"Nilipokuwa nikiwaeleza wazazi wangu waninunulie sare za shule na madaftari wanasema hawana hela maisha yao magumu, ndipo na mimi ikabidi niwe mtoro shule na kwenda kuchunga ng'ombe," anaongeza Sahani.

Aidha, anaeleza baada ya familia yao kuingizwa kwenye mpango huo wa kaya maskini, alinunuliwa sare za shule na mahitaji mengine sasa anafanya vizuri kitaaluma akishika nafasi ya 13 kutoka ya 50.

Helena Mtaki ni mwalimu mlezi wa Shule ya Wichamike, anasema TASAF imekomboa wanafunzi wanaoishi kwenye umaskini baada ya kuwapatia mahitaji ya shule yaliyowawezesha kuacha utoro.

Anasema mara baada ya kuona kuna baadhi ya wanafunzi wamekuwa watoro sugu, alifuatilia taarifa zao na kugundua kuwa ni wale wanaoishi maisha duni, walioshindwa kwenda shule sababu ukosefu wa sare za shule na hata zile walizokuwa nazo zimechanika na pia hawana fedha za kununua daftari kubwa kama kaunta zinazotumiwa na wanafunzi darasa la saba..

"Watoto hawa wana akili na wanafanya vizuri darasani mara baada ya kuhudhuria masomo bila kukosa kumekuwa na mabadiliko. Serikali inatoa elimu bure lakini baadhi ya familia maisha yao ni magumu na wamekuwa wakishindwa kuwahudumia watoto hasa upande wa mavazi, sare na hata chakula nyumbani." Anasema.

Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Wichamike, Respicius, anasema utoro shuleni umeisha kwa watoto hao wenye maisha magumu siyo kama zamani, mara baada ya TASAF kubadili mfumo wa maisha yao, ambapo wazazi wao kwa sasa wanajishughulisha na kilimo, pamoja na ufugaji mifugo kupitia fedha za TASAF.

Mmoja wa wazazi ambaye yupo kwenye mpango huo wa TASAF, Pili Maige mkazi wa Ntobo- Msalala, anasema kwa sasa maisha yake yamebadilika, ana miliki mbuzi sita, ana kuku na baadhi ameshauza, kwa ajili ya kuhudumia watoto mahitaji yao ya shule, pamoja na kununua chakula.

Anasema awali kabla ya kuingia TASAF mwaka 2015, maisha yake yalikuwa magumu na alikuwa akishindwa kuwatimizia watoto wake mahitaji hivyo kuamua kwenda nao kwenye mashamba binafsi kulima vibarua ili apate fedha za kuwanunulia sare za shule na madaftari, huku wakiwa tayari wameshakosa masomo kwa muda mrefu.

"Baada ya kupata ruzuku TASAF, nilianza kutunza akiba ya fedha huku nyingine nikitumia, ambapo baadae nilinunua kuku wawili, mbuzi jike ambaye ameshazaa. Nimeongeza mbuzi wengine na sasa wako tisa," anasema Maige.

Mratibu wa TASAF Halmashauri ya Msalala Elikana Zabloni, anasema kwenye halmashauri hiyo kuna walengwa 4,128, na mwaka jana (2020) kuanzia Agosti hadi Oktoba, wameshatoa Sh. milioni 256.

Anabainisha kuwa kabla ya kuwapa fedha hizo wanawapa elimu ya kuwekeza kwenye kilimo, na ufugaji ili wajikwamue kiuchumi.

Anasema kwenye utoaji wa ruzuku hiyo kuna masharti ya lazima ambayo ni pamoja na kuwa na Bima ya Afya Iliyoboreshwa (CHF), pamoja na kuwapeleka watototoni, kuwapa mahitaji yao, ikiwamo ununuzi wa sare za shule na mahitaji mengine ambayo Mwanafunzi anapaswa kuwa nayo.

Aidha anasema kutokana na fedha hizo mwisho wake, ndipo wanaamua kuwajengea uwezo walengwa namna ya kuzitumia kujikwamua kiuchumi, kwa kujikita kwenye shughuli za kilimo cha biashara na ufugaji wa mifugo, ili waendelee kupata fedha za kusomesha watoto wao licha ya mpango huo kufika kikomo.

"Hali ya maisha ya walengwa wa TASAF Msalala ni nzuri siyo kama zamani, ambapo kama ulivyoona kila kaya kuna mifugo na wengine shamba la kilimo cha biashara yakiwamo machungwa na pamba. Mazao yanauzwa ili kujipatia pesa zinazojenga nyumba bora,"anasema Zablon.



## TANESCO yatoa angalizo uharibifu wa miundombinu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUTOKONA na maji kuendelea kuingia kwa mita za ujazo kati ya 600 hadi 1,000 kwa sekunde katika mabwawa ya kufua umeme ya Mtera na Kidatu, Shirika la Umeme (TANESCO) limewata wakazi wa maeneo hayo wanaoendesha shughuli za kijamii kuchukua tahadhari ili kuepuka uharibifu wa miundombinu.

Baadhi ya wakazi wanaoishi pembezoni mwa mkondo wa maji yatokayo katika mabwawa ya kufua umeme ya Mtera na Kidatu, wamekuwa wakifanya shughuli za kilimo na ufugaji katika maeneo hayo jambo ambalo ni hatari hususani kipindi hiki cha mvua zinazoendekea kunyesha.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa kituo cha kufua umeme Mtera, Mhandisi Elias Mwalupilo, alipotembelea eneo hilo na kubaini maji kuendelea kuingia katika mkondo huo.

"Kutokana na kina cha maji kinazidi kuongezeka, itatulazimu hapo baadaye kama hali itaendelea kuwa hivi kupunguza maji yaliyozidi kwa kuruhusu kupita kwenye mkondo wake wa asili kwa ajili ya usalama wa miundombinu ya umeme pamoja na daraja," alisesema Mhandisi Mwalupilo.

Alisema Shirika linalazimika kuyapunguza maji yaliyozidi kina cha juu cha bwawa ambacho ni 698.50 kwa ajili ya usalama wa bwawa na mitambo ya kufua umeme ili iendelee kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhandisi Mwalupilo, alisema kutokana na mvua nyingi ambazo zilinyesha mwaka jana hasa Nyanda za Juu Kusini Mikoa ya Mbeya, Iringa na Njombe ambako, kuna vyanzo vingi vya maji ilipelekea bwawa la Mtera kupata maji mengi, hivyo uwepo wa mvua za wastani mwaka huu kumepelekea kina cha maji katika bwawa la Mtera kuongezeka.

Mhandisi Mwalupilo alivitaja vijiji vinavyotakiwa kuchukua tahadhari kwa upande wa mkondo wa Mtera ni Keseke, Idodoma wilayani Mpwapwa, kwa Kilolo ni Nyanzwa na Ruaha Mbuyuni, Wilaya ya Kilosa ni Malolo, Msosa na Kidai 'A' na 'B'.

# Siku 14 za wadaiwa Mfuko wa Pembejeo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ametoa siku 14 kwa uongozi wa Mfuko wa Pembejeo nchini kumpatia orodha ya wadaiwa yenye mchanganuo wa madeni na kiwango kinachodaiwa ili ufuatiliaji ufanyike kwa kuhusisha mamlaka za juu.

Bashe, alitoa maagizo hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na watumishi pamoja na viongozi wa mfuko huo. Alisema mfuko huo unatakiwa kuweka nguvu katika ukusanyaji wa madeni ya mikopo ambayo wamekopesha wakulima kwakuwa ni kiasi kikubwa cha fedha ambacho kipo nje.

"Kipaumbele chenu kwa sasa lazima kiwe ni kukusanya madeni ya mikopo mliyowakopesha wakulima tangu mfuko huu uanzishwe mwaka 1995 ni takribani Sh. bilioni 30 zipo nje na kiasi ambacho mmefanikiwa kukusanya hadi hivi sasa ni Sh. bilioni 10 pekee," alisema Bashe.

Kutokana na hali hiyo, aliuagiza uongozi huo kutumia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kudai madeni ya mikopo iliyokopeshwa kwa wakulima kiasi cha Sh. bilioni 20 na kuutaka mfuko kusitisha ukopeshaji kwa sasa.

**Kutokana na hali hiyo mfuko huo unatakiwa kuitumia TAKUKURU kudai madeni hayo kwa wakulima ambao yamekuwa ya muda mrefu.**

Aidha, alisema kuwa kutokana na hali hiyo mfuko huo unatakiwa kuitumia TAKUKURU kudai madeni hayo kwa wakulima ambao yamekuwa ya muda mrefu.

"Nawaomba mwandikie kwa Mkurugenzi wa TAKUKURU ili muwatumie TAKUKURU kudai fedha hizi kwani wao wako vizuri katika kudai madeni hawa wengine mtasumbuana tuu na mambo ya mahakamani,"alisema Bashe.

Kadhalika, Bashe aliagiza mfuko huo kusitisha utoaji wa mikopo hadi hapo utakapofanya marekebisho ya muundo wake.

"Mfuko huu tangu uanzishwe mwaka 1995 haujawahi kutengeza faida na hii ni kutokana na muundo wenu mnatoa mikopo lakini mlivyo kama siyo taasisi inayojihusisha na utoajiwa fedha," alisema Bashe.

Vile vile, alisema kuwa moja ya sababu inayochangia kiasi kikubwa cha fedha kupotea kutokana na mikopo chechefu ni kwa sababu ya kukosekana kwa bima ya mikopo.

"Kutokuwapo kwa bima ya mikopo kunasababisha sana fedha kupotea kutokana wakulima wakati mwingine kushindwa kurejesha kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na majanga mbalimbali hivyo kabla hamjaanza kutoa mikopo mingine mhakikishe kwanza mnakuwa na bima ya mikopo," alisema.

Kadhalika, Bashe aliutaka mfuko huo kuvunja mikataba yote waliyoingia na kampuni binafsi ya kudai madeni hayo kwa wakulima.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa mfuko huo, Festo Mhimba, alisema wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabia nchi kama vile mafuriko, ukame hali ambayo inachangia wakulima kushindwa kurejesha mikopo.

"Kikwazo kingine ni wadaiwa kuweka mazuio mahakamani wakati wa kufuatilia madeni kwa kuuza dhamana hali inayosababisha kuchelewa kwa marejesho kwa kuwa kesi huchukua muda mrefu," alisema Mhimba.

Hata hivyo, alisema kikwazo kingine ni dhana potofu iliyopo miongoni mwa wakopaji kuwa fedha ya serikali ni ruzuku hali ambayo hurudisha nyuma hamasa ya urejeshaji.




Afisa masoko Jiji la Dodoma, Jemes Yuna (kulia), akitoa maelekezo kwa wafanyabiashara wa ndizi mbichi wa soko la Bonanza kuzoa takataka zao za vifungashio vinavyoletwa toka nje ya mikoa badala ya kuziaacha sokoni hapo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Shekhe akemea wanaokaidi kutumia vitakasa mikono

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amekemea baadhi ya waumini wa dini ya Kiislamu wanaokataa kutumia vitakasa mikono kwa madai kuwa havina tofauti na vilevi.

Kiongozi huyo alisema hayo juzi wakati alipokuwa akitoa mawaidha ya swala ya Ijumaa kwenye Msikiti wa Gadafi jijini Dodoma.

Shekh Rajabu alisema kuwapo na baadhi ya waumini wanaovumisha kuwa vitakasa mikono ambavyo vinatumika kwa ajili ya kujilinda na maambukizi ya magonjwa ya mlipuko ikiwamo corona havifai kutumiwa kwa madai kuwa vina kilevi.

Aliwataka waumini wa msikiti huo katika kipindi hichi ambacho dunia inaendelea kupambana na ugonjwa hatari wa corona ni lazima kuendelea kuchukua taadhali na kuendelea kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya.

"Ndugu zangu Waislamu tupo katika kipindi cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona kutokana na hali hiyo, tuendelee kuchukua taadhari ya kiafya tuvae barakoa, tunawe mikono na kutumia vitakasa mikono huku tukimuomba Mungu kwa kila wakati..

"Kuna watu ambao wanasambaza uvumi na uzushi kwa kueleza kuwa vitakasa mikono vina kilevi ndani yake hivyo si sawa kwa kutumiwa, watu hao kwa kweli wanaonekana na wao waenezaji wa magonjwa haya .

"Hivyo mimi kama kiongozi wenu ninawasihi waumini na Watanzania kwa ujumla maneno hayo yapuuzeni kwani tayari kiwango cha alcohol iliyotengeneza vitakasa mikono haipo katika viwango vya pombe kama vile bia au konyagi tayari matumizi yake ni mengine kabisa"alisisitiza

Aidha, aliwahimiza waumini wa dini ya kiislam kuhakikisha wanakuwa wacha Mungu kwa kufanya mambo mema kutokana na maelekezo ya dini ya Kiislamu.

"Lazima tutumie vyema imani yetu kwa kumcha Mwenyezi Mungu na kuwa mabalozi waadilifu wa dini ya Kiislamu kwa kutenda matendo mema badala ya kufanya mambo ambayo hayana baraka na Utukufu kwa Mwenyezi Mungu," alisema.



# Adaiwa kuua mdogo wake wakigombea baiskeli

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamsaka, Frank Msafiri, mkazi wa Mwasanga jijini Mbeya kwa tuhuma za kumuua mdogo wake, Beny Msafiri (35), wakigombea baiskeli.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki katika Kata ya Mwasanga ambapo mtuhumiwa alimkata mdogo wake na kitu chenye ncha kali mguuni.

Alisema baada ya marehemu kukatwa alivuja damu nyingi iliyosababisha kifo chake wakati akikimbizwa hospitalini, na kwamba mtuhumiwa alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linashirikiana na vyombo mbalimbali kumsaka Frank, na watahakikisha anakamatwa popote atakapokuwa hata kama ni nje ya nchi, ili achukuliwe hatua za kisheria.

**Nawaomba wananchi popote watakapomuona mtu huyu watowe taarifa ili tumkamate na kumpeleka mbele ya vyombo vya sheria.**

"Nawaomba wananchi popote watakapomuona mtu huyu watowe taarifa ili tumkamate na kumpeleka mbele ya vyombo vya sheria," alisema Kamanda Matei.

Aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa maelezo kuwa ni kosa la jinai, na kwamba ikitokea watu wamekosana kuna mamlaka za kupeleka malalamiko.

Aliwataka viongozi wa Serikali pamoja na wa dini kuendelea kushirikiana na Jeshi hilo kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kutunza amani na utulivu kwenye maeneo yao ikiwemo kuepuka migogoro ya kifamilia.

Alitoa pole kwa familia ya marehemu na kuahidi kushirikiana nayo kuhakikisha mtuhumiwa anasakwa na kukamatwa.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa za siri wanapowaona watu ambao wanawadhania kuwa ni wahalifu ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uharifu wao kwenye jamii.

"Tumejipanga vyema kuhakikisha mkoa wetu unakuwa salama, ni wajibu wa wananchi kutupa ushirikiano ili tutekeleze hili kwa weledi, sasa wahalifu wote watafute kazi zingine za kujiingizia kipato halali," alisema Matei.

Katika hatua nyingine, aliwataka wananchi wanaofanya shughuli kwenye migodi kuchukua tahadhari kipindi hiki cha mvua kwa maelezo kuwa kuna hatari ya migodi hiyo kuporomoka na kusababisha madhara kwao.




Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (mwenye kofia), akikagua baadhi ya bidhaa zinazozalishwa na baadhi ya vijana wakati wa mafunzo kwa vijana ya kuwa wajasiriamali, ambayo yalianzishwa na Serikali ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Ndaki ya Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Viongozi wapewa jukumu la mazingira

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa Serikali mkoani Mbeya wameombwa kuwahamasisha wananchi kutunza mazingira, ikiwamo vyanzo vya maji kuhakikisha miradi ya maji inayotekelezwa inakuwa endelevu na inawasaidia wananchi kwa muda mrefu.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mjumbe wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-UWSA), Hilda Ngowi, wakati wa ziara ya Bodi hiyo kutembelea miradi ya maji iliyotekelezwa na mamlaka hiyo.

Alisema kwa sasa vyanzo vingi vya maji vimekuwa vikivamiwa na wananchi ambao wanafanya shughuli zao za kiuchumi ikiwamo kilimo, kuchungia mifugo pamoja na kukata miti kwa ajili ya shughuli mbalimbali hali ambayo inahatarisha vyanzo hivyo.

Alisema kwa sasa Mamlaka hiyo ina vyanzo vingi vya maji ambavyo vinasaidia wananchi kupata maji kwa asilimia 80 na kwamba endapo vyanzo hivyo vitaharibiwa kuna uwezekano maji yakapungua.

"Niwaombe sana viongozi wetu watusaidie kukabiliana na uharibifu wa mazingira, wananchi wapewe elimu ya kukabili mabadiliko ya tabianchi kwa kupanda miti," alisema Ngowi.

Kwa upande wake, Said Salmin, mjumbe, aliwataka wananchi kulipia bili za maji ili kuiwezesha Mamlaka hiyo kutekeleza miradi kwa kutumia mapato ya ndani .

Alisema Serikali imekuwa ikisisitiza taifa kujitegemea badala ya kutegemea misaada kutoka nje na kwamba mamlaka hiyo ni miongoni mwa taasisi ambazo zinajitosheleza kwa asilimia 100.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka hiyo, Edina Mwaigomole, aliwapongeza watendaji wa mamlaka hiyo kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maji viwango vinavyoendana na kiwango cha fedha zinazotengwa.

Alisema wataendelea kuhakikisha Mamlaka hiyo inajiendesha kwa kuhakikisha wananchi wanalipia Ankara za maji pamoja na kuboresha mifumo ya fedha.

# Chakula chasababisha utoro shuleni

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKOLE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Busoke wilayani Rungwe, inakabiliwa na utoro wa wanafunzi katika shule za msingi kutokana na kukosekana kwa chakula cha mchana kwa wanafunzi hao.

Ofisa Elimu wa Halmashauri hiyo, Matrida Mwampamba, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kilele cha maadhimisho ya wiki ya elimu ambapo alisema halmashauri hiyo ina jumla ya Shule za Msingi 62.

Alisema kati ya shule hizo ni 11 pekee ndizo zinatoa chakula kwa wanafunzi wote, 32 zimekuwa zikitoa kwa madarasa ya mitihani pekee huku zilizobakia zikiwa hazitoi kabisa chakula kwa wanafunzi hali ambayo inazorotesha taaluma.

"Suala hili la chakula shuleni limekuwa likisisitizwa kwenye vikao na mikutano mbalimbali, lakini mpaka sasa ni asilimia 66 pekee ya shule zote ndio chakula kinapatikana kwa wanafunzi, jambo hili limekuwa likisababisha utoro kwa wanafunzi kutohudhuria shuleni na wengine kutoroka baadhi ya vipondi," alisema Mwampamba.

Aidha Mwampamba alisema mbali na tatizo hilo, pia Halmashauri hiyo inakabiliwa na tatizo la upungufu wa miundombinu mbalimbali ya elimu ikiwemo vyumba vya madarasa, vyoo na nyumba za walimu hali na hivyo akadai kuwa juhudi kubwa zinahitajika kutatua matatizo hayo.

Alisema mpaka sasa upungufu wa vyumba vya madarasa kwa shule za msingi ni asilimia 17, vyoo asilimia 41, nyumba za walimu ni asilimia 77 na kwamba kwa upande wa madawati Halmashauri inajitosheleza na kuna ziada ya asilimia 23.5.

Hata hivyo, Mwalimu Mwampamba alisema Halmashauri hiyo imepiga hatua kubwa katika kukabiliana na mimba za ututoni kwa wanafunzi wa shule za msingi ambapo mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Disemba mwaka jana hakuna mwanafunzi aliyeripotiwa kupata mimba.

Alisema wamefanikiwa kutokana na elimu ambayo imekuwa ikitolewa kwenye jamii kuhusu madhara ya mimba hizo kwa watoto na kwenye jamii nzima kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Busokelo, Anyosisye Njobelo, aliwataka wenyeviti wa kamati za shule kushirikiana na walimu kuhamasisha wazazi kuchangia chakula ili wanafunzi wote kula chakula wakiwa shuleni.



## Wawakilishi sasa wataka kuimarisha mazao ya viungo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAANGALIZI wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 wamekumbushwa kuwashirikisha viongozi wa vyama vya siasa pamoja na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa wakati wa kuwasilisha taarifa zao za uangalizi wa mchakato huo.

Ushauri huo ulitolewa na Kaimu Mkurugenzi wa Uchaguzi Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Saadun Ahmed Khamis, wakati akipokea taarifa ya waangalizi wa kutoka Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar JUWAUZA.

Saadun alisema, waangalizi baada ya kukutana na tume hiyo, wanapaswa kukutana na wadau wengine wa uchaguzi wakiwamo vyama vya Siasa na Ofisi ya Msajili wa Vyama ili kuwasilisha mapendekezo na changamoto ambazo zinawahusu moja kwa moja wadau hao.

Aidha, Saadun alizidi kusema kuwa, tume hiyo kwa upande wake imeyapokea na kuahidi kuzifanyia kazi kwa kadri itakavyowezekana changamoto na mapendekezo yote yaliyowasilishwa na waangalizi wa uchaguzi ili kuona uchaguzi unaofuata unakuwa huru na wa kuaminika.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Saadat Haji, aliishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuingiza elimu ya wapiga kura katika mtaala wa elimu wa shule za sekondari ili kuwafanya wanafunzi kuwa na uelewa mkubwa wa masuala ya kidemokrasia katika uchaguzi.

Wakati, akiwasilisha taarifa fupi ya matukio yaliyojitokeza katika uchaguzi mkuu 2020 mtaalamu wa mawasiliano katoka JUWAUZA, Hawra Mohammed Shamte, aliipongeza Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kusimamia vyema uchaguzi huo na kuwashirikisha kikamilifu watu wenye mahitaji maalumu katika uchaguzi huo.

# Waziri awataka vijana, wanawake kujiajiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Uzini, Khamis Hamza, amewataka wananchi hususani vijana na wanawake kujiajiri katika kilimo na ufugaji badala ya kukaa na kusubiria ajira zinazotolewa na serikali.

Aliyasema hayo katika Kijiji cha Miwani Jimbo la Uzini Wilaya ya Kati Unguja wakati wa ziara ya viongozi wa Jimbo hilo ya kuwatembelea wananchi ili kusikiliza matatizo walionayo na kuyatafutia ufumbuzi.

Hamza alisema lengo la serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ya Jamhuri ni kuona wananchi wake wanakuwa na maendeleo kupitia rasilimali zilizopo nchini ili kujikwamua na umaskini.

**Zipo fursa nyingi za ajira kupitia kilimo na ufugaji wa kisasa na kuwahimiza wanawake na vijana kuunda vikundi...**

Alisema zipo fursa nyingi za ajira kupitia kilimo na ufugaji wa kisasa na kuwahimiza wanawake na vijana kuunda vikundi vitakavyozalisha mazao na mifugo mingi na kuwasaidia kujiongezea kipato cha kila siku.

Hamza alisema kupitia vikundi hivyo viongozi hao wa jimbo watasaidia kwa kuwapa mitaji na kuwatafutia mikopo isiyo na riba kutoka serikalini pamoja na kuwatafutia masoko ya uhakika kwa bidhaa watakazozalisha.

Mwakilishi wa jimbo hilo, Haji Shaaban, aliwataka wananchi kungana pamoja katika kuliombea taifa katika wakati huu ambapo dunia inapoteza maelfu ya watu kwa ugonjwa wa corona.

Aliwataka wananchi kuomba kupitia sehemu zao za ibada bila kujali tofauti za kidini kwa kufunga na kumlilia Mungu pamoja na kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo kwa kufuata ushauri unaotolewa na wataalamu wa afya.

Katika ziara hiyo viongozi hao walipata fursa ya kutoa misaada mbalimbali na kushiriki ibada ya kuliombea taifa amani katika Kanisa la Waadventista Wasabato liliopo Kiboje.



Mwakilishi wa Jimbo la Tumbatu, Haji Omar Kheri (kushoto), akiwa na Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib, wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaahidi kuboresha sekta ya elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Ali Juma, amesema serikali itahakikisha mchakato wa kuboresha elimu pamoja na kuwapo kwa sera bora ya elimu unazingatiwa.

Akizungumza katika kongamano la wadau wa elimu la kutoa maoni yao juu ya Sera ya elimu ya mwaka 2021 Mjini Unguja, Juma alisema lengo kuu ni kuona kila mwenye hoja na mawazo anatumia fursa hiyo kuyatoa ili nchi ipate dira mpya ya elimu ambayo itajenga misingi mizuri ya sekta hiyo .

Alisema wakati umefika wa kuhakikisha msingi wa kuwa na wataalam wazuri kwa fani zote unafanikiwa. Mkurugenzi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Wizara ya Elimu, Khalid Masoud Waziri, alisema ili kuboresha sera ya elimu inahitaji ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wa sekta hiyo kuhakikisha wanatoa maoni yao na kusaidia kufikia malengo.

Alisema kutokana na mabadiliko yanayojitokeza katika maendeleo ya dunia kuna umuhimu wa kufanya marekebisho katika sera iliyopo ili kupata ya elimu bora kwa taifa.

Kwa upande wake Katibu Mkuu mstaafu Wizara hiyo, Muhandisi Idrissa Muslim Hija, alisema ipo pia haja kuboresha elimu ya ufundi ili isaidie kufikia malengo.

Alisema bado kuna mitazamo ya baadhi ya watu kuona kuwa vyuo vya Mafunzo ya Amali ndivyo inastahili kuchukua wanafunzi waliofeli shuleni jambo ambalo siyo sahihi na kuwataka watu kutambua kuwa wanaochukuliwa ni wale wanaokuwa wamekidhi vigezo .

Akiwasilisha Sera ya elimu ya 2021, Ofisa Sera kutoka Wizara ya Elimu , Othman Omar Othman, alisema mfumo wa elimu ni utaratibu unaoonesha ngazi ya elimu ya Mwanafunzi anaopitia kuanzia ngazi ya awali hadi elimu ya juu.

Alisema mfumo ulioandaliwa sasa na Wizara hiyo umewekwa elimu ya awali ni miaka miwili, msingi miaka saba badala ya miaka sita, na sekondari ni wa miaka minne.

Alisema sera hiyo inaeleza kuwa elimu ya msingi inamsaidia mtoto kujua kusoma, kuhesabu na kuandika pamoja na kwamba elimu ya sekondari inasaidia kumjengea mtoto kuwa na stadi na maarifa.

Wakitoa michango yao wadau wa elimu walioshiriki katika kongamano hilo, waliiomba katika sera mpya kuongezwa vipengele ambavyo vitaitambua elimu ya ufundi kuwa ni ya lazima kwa wale wasiofaulu ili kuwajengea watoto mustakabali mzuri wa maisha yao ya badae.

Wakichangia kuhusu suala la matumizi ya lugha katika ufundishaji, wadau hao walisema ni vyema Kiswahili kikapewa kipaumbele katika kufundishia kwa elimu ya awali.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano :0713327613.

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**


## KUPOTEA KWA CHETI



**TERENCE KELVIN KIBANGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne pamoja na transcript yenye index namba **D.672/394** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **ST.MARY'S mwaka 2007**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa RB/38816/2021**

## KUPOTEA KWA PASSPOT



**TERENCE KELVIN KIBANGA** anatangaza kupotelewa na passpot ya kusafiria yenye namba **AB506989** Iliyotolewa na wizara ya uhamiaji mwaka **2018**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi,mahali ilipopotea

**DAR ES SALAAM.**

**Polisi taarifa RB/38816/2021**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI -TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 29/2021**
**Ombi la YUSUF AHMED MOHAMED kuteuliwa**
**Msimamizi wa mirathi marehemu OMARI MOHAMED DAWIL**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo **tarehe 2/3/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 17/2/2021**



## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL LULIKELA NTATIYE** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **mark II TOYOTA** yenye namba za usajili **T 591 ABH** chasisi namba **GX81318839** , yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi **Polisi taarifa M O R / M O R / R - B/96070/2021.**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, RAISSA COMPANY LTD** tutauza kwa mnada wa hadhara wa kiwanja, mali ya Mdaiwa Sugu. Irene Matiku Nyamtonga- kiwanja kilichopo Kijiji cha Kibiti Chalinze-Pwani.

Mnada utafanyika **Tarehe 8/03/2021**. Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo anaodaiwa. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

Mawasiliano fika ofisini kwetu Victoria **5th floor –DSM au piga no. 0652113262**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ndege za Boeing 777 zasitisha safari

**Denver, MAREKANI**

SHIRIKA la Ndege la United Airlines, limesema linasitisha ndege zake 24 aina ya Boeing 777 baada ya moja ya ndege hizo kupata hitilafu ya injini baada ya kuruka Jumamosi.

Ndege hiyo ya Boeing 777, iliyokuwa na abiria 231 na wafanyakazi 10, ilifanikiwa kutua salama katika uwanja wa ndege wa Denver na hakuna majeruhi walioripotiwa.

Mabaki ya ndege hiyo yalionekana kusambaa karibu na makazi ya watu.

Ikizungumzia tukio hilo, Japan imeyataka mashirika yote yanayotumia Boeing 777 zenye injini sawa ya Pratt & Whitney, 4000 kuepuka kuruka.

Boeing ilisema inaunga mkono uamuzi wa Japan na ilipendekeza kusimama kwa shughuli zote za Boeing 777 zenye injini kama hiyo wakati uchunguzi wa kuhusu tukio hilo ukiendelea.

Watengenezaji wa aina hiyo ya ndege walisema ndege 69 za Boeing 777 ziko kwenye matengenezo kote duniani zenye injini ya aina hiyo.

Ndege ya shirika hilo, nambari 328, iliyokuwa ikielekea Honolulu ilipata hitilafu kwenye injini yake ya kulia, Mamlaka ya Anga ( FAA) ilieeleza.

Shirika limetaka uchunguzi zaidi kufanyika kwa aina ya ndege ya Boeing 777 zenye injini ya Pratt & Whitney 4000 baada ya ajali hiyo.

Mmoja wa abiria alisema ndege ilikuwa ikitikisika hasa, aliliambia shirika la habari la AP kwamba rubani alikuwa akitoa tangazo wakati mlipuko mkubwa ukisikika. “Ndege ilianza kuyumba yumba sana, mara ikaanza kushuka chini,” David Delucia alisema.

Aliongeza kuwa yeye na mke wake waliweka stakabadhi za utambulisho mfukoni ili ndege ikianguka, waweze kutambuliwa.

Japan ilisema aina ya ndege zote za 777 zilizo na injini za Pratt & Whitney 4000 zinapaswa kuepuka kufanya safari, hii ni pamoja na kuruka na kutua.

Serikali pia iliamuru mashirika ya JAL na ANA kuacha kutumia ndege zake za Boeing 777 zenye injini ya Pratt and Whitney 4000.

Desemba mwaka jana ndege ya JAL ililazimika kurudi uwanja wa ndege wa Naha, kwa sababu ya kuharibika kwa injini ya kushoto.

Ndege hiyo ilikuwa na umri sawa na ndege ya United Airlines ya miaka 26 kutokana na tukio la Jumamosi.

Mwaka 2018, injini ya kulia ya ndege ya United Airlines ilivunjika muda mfupi kabla ya kutua Honolulu.

Kufuatia uchunguzi, Bodi ya Kitaifa ya Usalama wa Usafiri ilisema tukio hilo lilisababishwa na kuvunjika kwa mapanga ya feni.

***BBC***



Waandamanaji wanaopinga mapinduzi wakiwa wameinua mikono kwa kukunja ngumi, wakati wa mkutano karibu na Kituo cha Reli cha Mandalay, Myanmar, jana, ikiwa ni wiki ya tatu mfululizo wa maandamano kwenye miji mikubwa nchini humo, tangu jeshi lichukue nchi. **PICHA/AP**

# Rais Somalia atolewa ushiriki usuluhishi

**Mogadishu, SOMALIA**

RAIS wa Somalia amekatazwa kushiriki mazungumzo yoyote ya kutatua mzozo nchini humo.

Hiyo ni baada ya muhula wa kuwapo madarakani kuisha mwanzoni mwa Februari.

Bunge lilipanga kufanya uchaguzi Februari 8, ukacheleweshwa, kwa sababu wabunge wapya bado hawajachaguliwa.

Upinzani unamshutumu Farmajo kujaza wafuasi wake katika bodi ambazo huchagua wabunge.

Rais wa Somalia, Mohamed Abdullahi Mohamed, maarufu Farmajo, ambaye muhula wake wa miaka minne madarakani ulifikia kikomo mwanzoni mwa mwezi huu.

Hatakiwi kushiriki katika mazungumzo yanayolenga kutatua mzozo ambao umechelewesha kufanyika uchaguzi mkuu mpya wa nchi hiyo, serikali za majimbo mawili kati ya matano nchini Somalia zilisema Jumapili.

Ucheleweshaji huo umezidisha mivutano katika taifa hilo la pembe ya Afrika ambalo liliharibiwa na vita vya wenyewe kwa wenyewe na ambalo bado linapambana na uasi unaofanywa na kundi la kiislamu la Al-Shabaab.

Mara kwa mara kundi hilo hufanya mashambulizi mjini Mogadishu na kwingineko.

Serikali ya Jubaland, moja ya mikoa mitano ya Somalia ilisema kipindi cha Rais Mohamed Abdullahi Mohamed kuwapo madarakani kimeisha na anapaswa kujitoa katika mazungumzo yoyote juu ya mzozo huu.

***VOA***

# Raia Sudan kupewa posho kila mwezi

**Khartoum, SUDAN**

FEDHA za wafadhili kwa ajili ya mpango unaolenga kulipa posho za kila mwezi za dola tano, kwa raia wengi wa nchi ya Sudan zilitolewa kwa wizara ya fedha kuanzia jana.

Hatua hiyo ni baada ya nchi hiyo kuridhia kupunguza thamani ya sarafu yake, Gavana wa Benki Kuu ya Sudan alisema.

Kupunguzwa kwa thamani ya paundi ya Sudan ni moja ya mageuzi magumu yaliyopendekezwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), ili kuisaidia nchi hiyo kupata nafuu ya kulipa deni lake na kuvutia wawekezaji.

Kutolewa kwa dola milioni 400 kwa ajili ya awamu ya kwanza ya mpango huo, kulicheleweshwa kutokana na wasiwasi kuwa thamani kamili ya posho hizo ingepungua kabisa chini ya kiwango cha ubadilishanaji wa sarafu ambacho hakijafanyiwa mageuzi.

Mamlaka nchini Sudan, imetoa wito kwa raia kuwa na uvumilivu wa mageuzi ya kisera yanayofanyika kwa sasa, kwamba lengo lake kuu ni kutetea maslahi ya raia wake.

***RFI***

# Vifo ebola vyaongezeka DRC

**Kinshasa, DRC**

WATU wanne wamepoteza maisha baada ya kuambukizwa virusi vya ebola, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku wataalamu wa afya katika eneo hilo wakisema raia wanakataa masharti ya kudhibiti virusi hivyo.

Katika mkutano na waandishi wa habari kwenye mji wa Butembo jimboni Kivu Kaskazini Mashariki mwa nchi hiyo, Waziri wa Afya wa Mkoa, Dk. Nzanzu Salita, alisema kuwa kati ya wagonjwa sita waliokuwa wamelazwa katika hospitali kwenye mji huo, baada ya kuthibitishwa kuwa na virusi vya ebola wanne walifariki.

Miongoni mwa wagonjwa wanne waliokufa ni mwendesha pikipiki mmoja ambaye inadaiwa alimsafirisha mgonjwa wa kwanza aliyeaminiwa kupatwa na ebola kutoka eneo la afya la Biena, Mwenyekiti wa Atamov, Kamati ya Waendesha pikipiki, Mumbere Misisa Jackson, alisema.

Ili kuzuia kuenea kwa virusi vya ebola, Waziri wa Afya mkoani Kivu Kaskazini aliongeza vikao vya uhamasishaji vinaendelea kutoa matunda.

Dk. Salita alitoa wito kwa wananchi katika eneo hilo kuchukua tahadhari zaidi wakati serikali ya mkoa huo ikiendelea na mapambano dhidi ya COVID-19.



# CONTE

## MAMBO YAMNYOOKEA SERIE A

**MILAN, Italia**

ANTONIO Conte anahisi Inter Milan ilionyesha "kiwango cha kuvutia zaidi" wakati wakibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya AC Milan, huku akiwasifia Christian Eriksen na Ivan Perisic.

Nerazzurri hao wamepaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa pointi nne baada ya ushindi huo wa Jumapili, huku Lautaro Martinez akifunga mabao mawili katika kila kipindi pale katika dimba la San Siro.

Romelu Lukaku alifunga bao lake la 17 kwenye ligi hiyo msimu huu na kukamilisha ushindi huo, wakati akielekea kuwa mchezaji wa kwanza kuifunga Inter katika mechi nne mfululizo za 'dabi' ya jiji moja la Milan tangu mwaka 1950.

Kwa Conte, yeye alifurahia ushindi huo kwa kusema kikosi chake kilionyesha kiwango cha kuvutia sana.

"Hongera kwa vijana, wameonyesha kiwango cha kuvutia sana," alisema Conte.

"Ni mechi iliyokuwa bora kabisa, ambapo walicheza vizuri kwa kufuata maelekezo yangu. Na nina furaha kwa sababu vijana walistahili ushindi."

Lakini Eriksen na Perisic, wachezaji wawili ambao wanahusishwa na mpango wa kuondoka klabu hapo, walikuwa kwenye kiwango bora zaidi kilichomvutia Conte.

" Christian na Ivan wamekuwa, ni wachezaji ambao najisikia fahari kuwa nao, kwa hakika kabisa walikuwa kwenye kiwango bora kabisa."

# United yakaribia kumsajili Donnarumma

**MANCHESTER, England**

GOLIKIPA wa AC Milan, Gianluigi Donnarumma amefikia makubaliano ya awali ya kujiunga na Manchester United, kwa mujibu wa Todo Fichajes.

Juventus, Bayern Munich, Paris Saint-Germain na sasa Manchester United zote zimeripotiwa zinamwania kipa huyo wa kimataifa wa Italia, Donnarumma.

Akiwa ndio kwanza anakaribia kutimiza umri wa miaka 22, Donnarumma ameripotiwa anakaribia kukamilisha dili na kujiunga na mashetani wekundu wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.


Ripoti hizo zinadai dili hilo litamfanya Donnarumma kuwa golikipa anayelipwa mkwanja mrefu zaidi duniani.

United wamekuwa na tatizo la golikipa msimu huu, huku kipa wao namba moja, David de Gea akifanya makosa mengi, huku Dean Henderson akicheza mechi chache.

**Donnarumma, ambaye atasherehekea siku yake ya kuzaliwa Al hamisi kwa kutimiza umri wa miaka 22, amekuwa golikipa mwenye umri mdogo zaidi kwenye historia ya Serie A kufikisha mechi 200 alizocheza wakati Milan wak ichezea kichapo cha mabao 3-0 Jumapili kutoka kwa Inter.**

Mkataba wake wa sasa na Rossoneri unamalizika mwishoni mwa msimu huu na amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa kubwa duniani.

# Guardiola ashangaa kiwango cha City



**LONDON, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema anakishangaa kikosi chake kuendelea kuwa kwenye kiwango cha juu "wakati kila mmoja akiwa kwenye wakati mgumu duniani" baada ya kuendeleza ushindi wa 18 katika mechi dhidi ya Arsenal.

City waliibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliopigwa kwenye dimba la Emirates, juzi Jumapili.

Vinara hao wa Ligi Kuu England, hivi sasa hawajapoteza pointi yoyote tangu Desemba 15, mwaka jana na wanaongoza kwa tofauti ya pointi 10 kileleni mwa msimamo, huku zikiwa zimesalia mechi 13.

Kama ilivyo kwa timu nyingine, wamekuwa na majanga kadhaa ikiwapo mlipuko wa virusi vya corona, pamoja na majeruhi, lakini bado wapo kwenye kiwango bora.

Guardiola amesema: "Ninashangazwa na hamasa yao na wakati kila mmoja yupo kwenye wakati mgumu, timu zote kwenye ligi zinapoteza pointi, sisi tuko imara na katika kiwango kile kile na sikutarajia hilo.

"Watu wanazungumza na kuzungumza kuhusu rekodi na ushindi, lakini ili ufanye hivyo unatakiwa kushinda mechi nyingi, nyingi sana.

"Sio tu kuhusu kushinda mechi tatu au nne kwa sababu hili ni ngumu katika kuweka rekodi."

Bao hilo pekee kwa City kwenye mchezo huo lilifungwa na Raheem Sterling baada ya kumzidi akili Rob Holding na kuitumia vizuri krosi ya Riyad Mahrez.

Wao Arsenal wapo nafasi ya 10 wakipitwa pointi sita kwenye sita bora.




# MESSI

## AWEKA REKODI MPYA LALIGA

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi ameweka rekodi mpya kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa kucheza mechi nyingi zaidi ya 506.

Awali Messi aliifikia rekodi iliyowekwa na mchezaji mwenzake wa zamani wa klabu hiyo, Xavier Hernandez ambaye amecheza mechi 505 kwenye ligi hiyo.

Messi alifunga bao katika mchezo huo wa 506 wa ligi wakati walipolazimishwa sare ya bao 1-1 na Cadiz pale kwenye dimba la Camp Nou.

Messi aliwaweka mbele Barcelona katika dakika ya 32 ya mchezo kwa njia ya penalti kabla ya Alex Fernandez kuisawazishia Cadiz dakika za mwisho kwa mkwaju wa penalti pia.

Endapo Barcelona wangepata ushindi hapo jana wangekuwa wameachwa alama sita na Atletico Madrid wanaoongoza katika msimamo wa ligi hiyo.

# DILI LA WIJNALDUM KWENDA BARCA LAYEYUKA




**LIVERPOOL**

LILE saga la chinichini la kiungo wa Liverpool, Georginio Wijnaldum kuhitajika na klabu ya Barcelona linaonekana halina nguvu tena.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, Barcelona haina uwezo wa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi kwa sasa, kwa sababu za kiuchumi.

Kama zilivyo klabu nyingi barani Ulaya, mlipuko wa virusi vya corona umezifanya kuyumba kiuchumi.

Hadi sasa Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30 hajazungumza chochote na Liverpool juu ya kuongezewa mkataba mpya.

Mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu na yeye mwenyewe ameshaonyesha wazi kwamba, hana mpango wa kuendelea kubakia hapo kwenye dimba la Anfield.

Kocha wa sasa wa Barcelona, Ronald Koeman ni raia mwenzake wa Uholanzi na anatajwa kwamba anamwania kiungo huyo ili aungane naye pale Barcelona.

Lakini kutoka na hali halisi ya kiuchumi, huku klabu hiyo ikielekea kwenye uchaguzi wa urais, dili hilo linaonekana kuwa kwenye wakati mgumu kukamilika kipindi cha majira ya joto kijacho.

# SPURS YATOA MSIMAMO KUHUSU KANE

**LONDON, England**

TIMU yoyote itakayotaka kumsajili, mshambuliaji na nahodha wa Tottenham Hotspur, Harry Kane itatakiwa kulipa kiasi cha pauni milioni 150.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Tottenham, Daniel Levy akinukuliwa na vyombo vya habari vya England, yupo tayari kumuuza Kane, lakini si chini ya pauni milioni 150.

Kane mwenye umri wa miaka 27 ambaye ni mfungaji bora wa Spurs kwa sasa, amekuwa akihuishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo.

Klabu za Manchester United na Manchester City zimekuwa zikitajwa kumwania nahodha huyo wa Timu ya Taifa ya England.

Kane ambaye analipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, sasa anaweza kuletewa ofa mezani baada ya mwenyekiti wake huyo kuweka hadharani bei yake hiyo.

Mfungaji huyo bora wa michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 nchini Urusi, alishawahi kunukuliwa akisema kwamba, hawezi tu kukaa Spurs, kwani anahitaji kutafuta timu ambayo inashinda mataji.

Tottenham licha ya kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, lakini haijatwaa taji lolote kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni, na Kane anataka kucheza kwenye timu inayowania mataji.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO AFUNGUKA KINACHOITESA SPURS

●●●Mreno huyo aweka wazi kuna matatizo ndani na kikosi na hawezi kuyamaliza peke...

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amesema kikosi chake "kina matatizo na siwezi kuyamaliza mwenyewe" lakini haamini kama Spurs ipo kwenye mgogoro baada ya kufungwa na West Ham.

Kipigo hicho cha 2-1 ni kichapo chao cha tano katika mechi sita za Ligi Kuu England, kiliiacha Tottenham kwenye nafasi ya tisa katika msimamo wa ligi hiyo, pointi tisa nyuma ya wanaoshika nafasi ya nne wagonga nyundo hao wa London.

Michail Antonio na Jesse Lingard kila mmoja alifunga bao moja kabla ya Lucas Moura kuifungia Spurs goli la kufutia machozi.

"Siwezi kusema tupo kwenye mgogoro," amesema Mourinho wakati alipoulizwa kuhusu kiwango cha spurs.

"Naweza kusema ni mbaya, mbaya sana, kucheza bila kupata matokeo. Tunapoteza mechi nyingi sana."

Magazeti ya Jumapili yaliripoti kwamba, kibarua cha Mourinho kinaweza kuwa shakani kama angefungwa na West Ham.

Mshidi huyo mara mbili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya amekuwa akishutumiwa na mashabiki wa Spurs kwa namna anavyopanga timu na matokeo wanayoyapata.

Lakini alipoulizwa kama kiwango kibovu cha Tottenham kinatokana na aina ya uongozi wake, Mourinho alijibu: "Hapana, hapana kwa kweli. Staili yangu ya ukocha na benchi langu la ufundi ipo wazi kabisa na ni bora.

"Nimefikiri kwa muda mrefu, muda mrefu sana, tuna tatizo kwenye timu na siwezi kulitatua mimi mwenyewe peke yangu kama kocha."

## KWA UFUPI

### HAALAND ATAJA DAU

STRAIKA wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland ambaye ana umri wa miaka 20, ameziambia klabu za England anataka kiasi cha pauni milioni 78 kama zinataka kumsajili. ***(Star)***

### PEARSON ANUKIA BRISTOL

KOCHA wa zamani wa Leicester na Watford, Nigel Pearson, yupo kwenye nafasi nzuri ya kuchukua nafasi ya kuinoa Bristol City baada ya kufikia pazuri kwenye mazungumzo yao. ***(Bristol Post)***

### DONNARUMMA KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United inafikiria kutoa ofa kwa AC Milan kwa ajili ya kumsajili golikipa wake na nyota wa Timu ya Taifa ya Italia, Gianluigi Donnarumma (21) . ***(Fichajes, via Team Talk)***

### SULE AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA imeripotiwa kuanza mazungumzo na Bayern Munich juu ya uwezekano wa kumsajili kwa pauni milioni 25.9, mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Niklas Sule, mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes, via Caught Offside)***

### BAYERN KUMBANA SULE

MKURUGENZI Mtendaji wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amethibitisha wataongeza mkataba wa beki wao, Niklas Sule ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Football London)***

### ZAHA AOMBA KUONDOKA

WINGA wa Crystal Palace, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 28, anajiandaa kuwasilisha maombi ya kuondoka klabuni hapo kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Todo Fichajes)***

### KASSOUNOU SOKONI

ARSENAL imeweka wazi inafanya mchakato wa kuwania saini ya kiungo wa Club Brugge na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Odilon Kossounou ambaye ana umri wa miaka 20 ifikapo kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### DRAGUSIN KUTUA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inamfuatilia kwa karibu mlinzi wa kati wa Juventus na Timu ya Taifa ya Romania chini ya umri wa miaka 21, Radu Dragusin (19), ambaye pia anawindwa na Tottenham na Newcastle. ***(Corriere dello Sport, via Sport Witness)***

### LIVERPOOL KUMTOA MINAMINO

LIVERPOOL inaweza kutoa ofa kwa kiungo wa Japan, Takumi Minamino mwenye umri wa miaka 26, kwa kubadilisha na winga wa Sevilla na Timu ya Taifa ya Argentina, Lucas Ocampos (26). ***(La Razon, via Star)***

### NEUHAUS ATAJWA LIVERPOOL

HATIMA ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Florian Neuhaus ambaye ana umri wa miaka 23 ndani ya kikosi cha Borussia Monchengladbach yapo shakani, baada ya wiki za hivi karibuni kuhusishwa na Liverpool. ***(Goal)***

### MILAN, WEST VITANI

WEST Ham itaingia kwenye mbio moja na AC Milan kipindi cha majira ya joto kinachokuja katika kuwania kumsajili fowadi wa Sevilla na Morocco, Youssef En-Nesyri mwenye umri wa miaka 23. ***(Il Milanista, via Sport Witness)***

HABARI MICHEZO

# KONGAMANO LA SOKA LAMREJESHA SVEN DAR

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Sven Vandenbroeck, anatarajiwa kurejea nchini kwa ajili ya kushiriki kongamano la soka linalotarajiwa kufanyika Machi 18 na 19, mwaka huu kwenye Ukimbi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sven, raia wa Ubelgiji alitangaza kuachana na Simba hivi karibuni na sasa amejiunga na klabu ya FAR Rabat ya Morocco.

Akizungumza na jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Afrisoccer, Peter Simon, alisema maandalizi ya kongamano hilo yamekamilika na linatarajiwa kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa soka kutoka nchi mbalimbali akiwamo kocha huyo wa zamani wa Simba.

Simon aliwataja baadhi ya wageni wengine waliothibitisha kuhudhuria kongamano hilo ni pamoja na mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Senegal, Khalilou Fadida ambaye aliwahi kuichezea klabu ya Bolton Wanderers na Inter Milan, Marcos Pelegrín kutoka Afrika Kusini ambaye ni Mwakilishi wa Laliga na Mshauri wa Yanga, Senzo Mbatha.

Wengine watakaoshiriki ni Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, Mulamu Nghambi ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Simba, Abdulkarim Amin 'Popat' kutoka Azam FC na Mwenyekiti wa Chama cha Soka cha Wanawake Tanzania (TWFA), Amina Karuma.

"Mkutano huo utakuwa na wadau mbalimbali wa soka kutoka ndani na nje ya nchi, na lengo la kongamano hilo ni kutengeneza jukwaa la kuwawezesha wadau kujifunza na kubadilishana ujuzi na uzoefu."

"Pia kuainisha fursa mbalimbali za kibiashara na kujadili mambo muhimu yanayohusu maendeleo ya mpira wa miguu na kutengeneza uhusiano na ushirikiano," alisema Simon.

Alisema kongamano hilo litasaidia wadau wa hapa nchini kujifunza mbinu mpya za uendeshaji wa soka kupitia kwa wageni ambao nchi zao zimepiga hatua katika mchezo huo.

Aliongeza walengwa wa kongamano hilo la kwanza la kimataifa ni wadau wote wa soka hapa nchini wakiongozwa na Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Kamati za Michezo za Mikoa na Wilaya, TFF, Bodi ya Ligi, klabu zote za soka, makocha na wachezaji wa zamani.

"Pia ni jukwaa muhimu kwa 'maskauti', waandishi wa habari za michezo na vituo vya soka," Simon aliongeza.

Alimtaja mgeni rasmi katika kongamano hilo atakuwa ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa huku Katibu wake, Hassan Abbas atafungua kongamano hilo.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Afrisoccer, Peter Simon (kulia), akizungumza kuhusu maandalizi ya kongamano la kujadili maendeleo ya mpira wa miguu nchini linalotarajiwa kufanyika mwezi ujao, hapa jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Mwakilishi wa Laliga katika nchi za Tanzania na Rwanda, Alvaro Paya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Biashara United bado yaiota Simba

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuichapa Ruvu Shooting mabao 3-0 katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa juzi, nahodha wa Biashara United, Abdulmajid Mangalu, amesema kikosi chao kimeendelea kuimarika lakini 'wanawaza' pointi walizopoteza dhidi ya mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba kutoka jijini Dar es Salaam.

Biashara United yenye rekodi nzuri inapocheza kwenye Uwanja wa Karume Mjini Musoma ilikubali kulala bao 1-0 dhidi ya Simba wiki iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mangalu alisema mabeki wa timu hiyo hawakuwa makini katika mchezo huo, ambapo iliwaruhusu Simba kuondoka na pointi tatu.

Mangalu alisema wanashukuru makosa hayo yamemalizika na sasa wanadhamiria kuendelea kupata matokeo chanya katika mechi zinazofuata za ligi hiyo ambayo iko kwenye hatua ya lala salama.

"Leo (jana), sijafanya mazoezi, nilipata tatizo, lakini nina imani nitarudi uwanjani mapema, wachezaji wenzangu wanaendelea kujifua kwa sababu tumeweka malengo ya kumaliza msimu katika nafasi za juu, tunaamini tutafanikiwa kutimiza ndoto zetu," alisema Mangalu.

Aliongeza wachezaji wamedhamiria kuendelea kupambana katika mechi zote zilizobakia na wanaamini watapeperusha vizuri bendera ya mkoa wao.

Alisema pia wanawashukuru mashabiki wao kwa kuendelea kuwapa 'sapoti' katika kila mechi wanayocheza nyumbani na wasichoke kuwaombea kuvuna pointi tatu kwenye michezo ijayo.

## Kipanga yaongeza mikakati Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa Kipanga, Rashid Lato, amesema timu yake itaongeza mikakati kwa ajili ya kuhakikisha inafanya vizuri na kutimiza malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu yanatimia.

Lato aliliambia gazeti hili wamejipanga kusaka ushindi katika kila mechi kwenye hatua hii ya lala salama ingawa wanafahamu michezo yote itakuwa migumu na yenye ushindani.

Kocha huyo alisema timu zote zinazoshiriki ligi hiyo zinacheza soka la ushindani na zinajituma ili kujiweka kwenye nafasi salama. "Mzunguko wa lala salama kwetu tunauona ni wakati wa mapambano, tunafahamu tuna makundi ya aina tatu, na kila kundi linapambana ili kufanya vizuri," alisema Lato.

Alisema kwa timu ambazo pia zinahitaji kutwaa ubingwa ushindani huongezeka na wao hawakati tamaa katika kuongeza nguvu na kasi kwenye michezo hiyo ili malengo yao yasipotee.

"Tunaenda kuanza mzunguko mgumu sana, kuna timu zinazohitaji kubaki kwenye daraja hili nazo hazihitaji kupoteza michezo muhimu, ila vita ipo zaidi kwa timu ambazo zinataka kujinasua na janga la kushuka daraja, hizi huwa zinabadilika sana katika mzunguko wa pili na ukifanya masihara zinaweza zikakuharibia hesabu zako," alisema Lato.

## KMC yajiimarisha kuwafuata Coastal

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuibuka na ushindi dhidi ya Kagera Sugar, kikosi cha KMC kinaendelea kujiimarisha na mazoezi kwa ajili ya mechi yao ya Kombe la FA na michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayofuata hivi karibuni.

KMC inatarajia kuikaribisha Kurugenzi FC katika mechi ya Kombe la FA na baadaye itasafiri kuwafuata Polisi Tanzania na Coastal Union jijini Tanga.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa KMC, Christina Mwagala, aliliambia gazeti hili kikosi cha timu hiyo kilianza mazoezi yake jana ili kuwajenga zaidi wachezaji wao kwa ajili ya kupambana kusaka ushindi kwenye mechi zinazowakabili.

Mwagala alisema wanafahamu sasa ligi imeingia kwenye hatua ngumu na yenye ushindani, hivyo wanatakiwa kujiimarisha kila idara.

"Tunajiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho itakayochezwa Ijumaa dhidi ya Kurugenzi kutoka Simiyu, sisi ndio wenyeji na mchezo utapigwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, pamoja na mambo mengine vijana wa Kino Boys wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri na kusonga mbele," alisema Mwagala.

Aliongeza wanahitaji kupata ushindi ili waelekee ugenini jijini Arusha kuwavaa Polisi Tanzania wakiwa imara na vile vile watakapokwenda Tanga kukutana na Coastal Union Machi 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani.

Michezo

Jumanne Februari 23, 2021

Nipashe



## MOURINHO AFUNGUKA KINACHOITESA SPURS

HABARI UK 22



Wachezaji wa Simba wakiwa kwenye mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly kutoka Misri itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, AL AHLY DK. 90 KUAMUA

●●●Matola, Bocco waahidi watafanya kila njia ili kuendeleza ubabe nyumbani...

**Na Adam Fungamwango**

VITA kamili ya Wawakilishi wa Tanzania katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya wenyeji Simba dhidi ya Al Ahly kutoka Misri inatarajiwa kufanyika leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Simba itawakaribisha vigogo hao wa Afrika ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa bao 1-0 ugenini katika mechi yake ya kwanza ya Kundi A dhidi ya AS Vita ya Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ni mechi ambayo inatarajia kuvuta hisia za mashabiki wengi wa soka barani Afrika, ambao macho na masikio yao yataelekezwa Tanzania kuangalia nini kitatokea baina ya timu hizo mbili.

Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola amekiri mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wanaocheza wote ni mabingwa, lakini wamejipanga kufanya kila njia ili kupata ushindi nyumbani.

"Siyo mechi rahisi. Hii ni Ligi ya Mabingwa, lakini tumejipanga. Tunakutana na timu nzuri, kubwa na bora zaidi, lakini tumejipanga kupata ushindi. Ninachoweza kuwaambia Watanzania hatuna majeruhi hata mmoja, hili ndilo tunalojivunia, hivyo tuna uwanja mpana wa kuchagua kikosi chetu kwa ajili ya kupambania ushindi," alisema Matola.

Nahodha na mshambuliaji wa timu hiyo, John Bocco ambaye alikuwa majeruhi kwa muda mrefu na sasa yuko fiti, alisema kikosi chao kimejipanga vyema kuondoka na ushindi, licha ya kwamba wanawaheshimu wapinzani wao.

"Tumejipanga vizuri, tunakwenda kucheza tukiwa na morali, tunawaheshimu wapinzani, ni wazoefu na ni wakubwa Afrika, lakini tunaamini mbinu tulizozipata kutoka kwa walimu wetu, Bocco alisema.

Kocha Mkuu wa Al Ahly, Pisto Mosimane, alisema wanakumbuka kipigo walichokipata kwenye mechi ya mwaka 2019, hivyo wamefanyia kazi makosa waliyoyafanya na wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa.

Hata hivyo kocha huyo amelalamikia hali ya joto ya Dar es Salaam, na kusema pamoja na mazingira hayo, wapinzani wao wako vizuri na wao watapambana kupata matokeo mazuri. Mara ya mwisho timu hizo kukutana kwenye uwanja huo ilikuwa ni Februari 12, mwaka juzi, katika mechi ya Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi ambapo Simba ilishinda bao 1-0, shukrani kwa mshambuliaji wake Mnyarwanda Meddie Kagere ambaye bado yupo kwenye kikosi cha Wekundu wa Msimbazi.

Hata hivyo, Simba itakuwa na kumbukumbu ya kuchapwa mabao 5-0 kwenye mechi ya kwanza ya kundi hilo, iliyochezwa Februari 2, mwaka 2019, nchini Misri.

Mara ya kwanza zilikutana mwaka 1985 kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika nchini Tanzania kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, Simba ikishinda mabao 2-1, ya Zamoyoni Mogella na Mtemi Ramadhani, Mohamed Al Khatib 'Bibo' akiifungia bao la kufutia machozi, Al Ahly wakiwa ni mabingwa watetezi wa michuano hiyo.

Mara ya mwisho Simba kupoteza mechi ya kimataifa kwenye ardhi ya nyumbani ni miaka saba iliyopita. Ilikuwa ni Februari 17, 2013, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Recreativo do Libolo ya Angola, ikiwa ni katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Al Ahly ndio wanaongoza katika msimamo wa Kundi A wakifuatiwa na Simba, AS Vita na El Merreikh ya Sudan ambayo ilichapwa mabao 3-0 katika mechi yake ya kwanza.

## MASTRAIKA YANGA WAMVURUGA KAZE

**Na Saada Akida**

LICHA ya timu yake kuendelea kushikilia rekodi ya kutopoteza mechi katika za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu 2020/21 unaoendelea, Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, amesema bado ana kazi ya ziada ya kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

Kaze alisema anaendelea kufanyia kazi upungufu uliyomo katika safu hiyo kwa kuongeza utulivu na umakini wa kutumia vyema nafasi wanazozitengeneza za kufunga mabao.

Kaze alisema pia anahitaji kuona washambuliaji wake wanakuwa watulivu wanapokuwa jirani na lango la mpinzani ili kujihakikishia ushindi mnono na mapema.

"Hatuwezi kupata ushindi bila kufunga, tunatakiwa kuwa makini hasa katika nafasi tunazotengeneza kuhakikisha tunafunga mabao ili kuendelea kujiimarisha zaidi, kuendelea kubaki hapa juu tulipo, tunatakiwa kupambana na kila timu bila kujali nafasi na jina la mpinzani ambaye tunakutana naye," alisema Kaze.

Yanga itaikaribisha Kengold katika mechi ya mzunguko wa nne wa Kombe la FA itakayochezwa Jumamosi jijini.

## NAMUNGO KUNDI LA 'KIFO' AFRIKA

**Na Mwandishi Wetu**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC imepangwa katika 'kundi la kifo' endapo itasonga mbele kwenye michuano hiyo.

Namungo 'imenusa' hatua hiyo baada ya kupata ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya CD Agosto ya Angola katika mchezo wake wa kwanza wa ugenini uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa jana jijini Cairo, Misri, Namungo au klabu hiyo ya Angola imepangwa katika Kundi D pamoja na Raja Casablanca ya Morocco, Pyramids (Misri) na Nkana FC ya Zambia.

Mechi ya marudiano kati ya Namungo dhidi ya CD de Agosto itachezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kuamua michezo yote miwili ifanyike Tanzania.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002